# CONSITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, GARSEN CONSTITUENCY, HELD AT KIPINI DO's OFFICE

## ON

# 2nd MAY, 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, GARSEN CONSTITUENCY, HELD AT KIPINI DO'S OFFICE ON THURSDAY, 2ND MAY, 2002**

**Present:**

1. Com. Charles Maranga
2. Com. Mutakha Kangu
3. Com. Alice Yano

**Secretariat Staff in Attendance**:

1. Programme Officer – Hassan M. Muhamed
2. Asst. Programme Officer – Beatrice M. Gikonyo
3. Verbatim Recorder – Irene Karei
4. Sign Language Interpreter – Christine Ondicho
5. District Co-ordinator – Bw. Omar Abdalla Dhadho

**Th**e meeting was called to order at 9.00 a.m. with Com. Maranga in the Chair**.**

Prayers were said by Salim Ali Hirbai.

**Salim Ali Hirbai :** Ee Yaradhi utuongoze. Kenya yetu, ututilie baraka haya matakwa yetu ambawo mambo tumeanza leo. Ambawo Mungu aututilie Baraka. Mungu atutilie Neema. Mungu atupe Rehema. Mungu atujalie kwa kila heri. Atuwapatie kila la mashari. Ee Allah, Amina. Wafuana. Wakufiliana. (The rest in Islamic).

**Com. Maranga**. Basi namshukuru Mzee Salim. Lakini kabla sijaendelea ningetaka Bw. Omar uweze kusema machache kuhusu kikao hiki .

**Bw. Omar** – Basi Wananchi watukufu, mimi jina langu naitwa Omar Abdalla Dhadho, ndiye Co-ordinator wa Tume ya mageuzi ya Katiba, Wilayani Tana River. Tuna mshukuru Mwenyezi Mungu kwasababu ametuwezesha kufika kwenu. Leo ikiwa ni kongamano la Tume la kutowa maoni. Kwa hivyo ningependa kutambua Com. Dr. Charles Maranga, Com. Mutakha Kangu, Programme Officer Bw. Hassan na wafanyi kazi wa Tume ambawo wamembatana nawo. Area Councillor Yahya, Ma Chiefu viongozi wa Tabaki mbali mbali wananchi kwa jumla. Karibuni kwa mukutano wetu wa leo na kabla hatuja anza tuta

fanya shuhuli moja ya haraka sana, kuwatambulisha wale watu ambawo kuamba tunafanya nawo katika Committee Members na kwa sababu Mkuu wa Tarafa ayuko, ambaye yuko ni Chief wa Kipini, na yeye tuta mpa nafasi kwaku muakilisha mku wa wilaya aweze kwa kutukaribisha rasmi hapa kwake na awaseme majina ya ma Chief wenzake na mimi nitafanya utangulizi wa Kamati ya sehemu wa wakilishi Bungeni ya Garsen Constituency. Halafu turudishwe usukani kwa ma Commissioners ili watueleze namnagani tutatoa maoni na utaratibu gani utakao fuata kwa ajili ya kukusanya maoni yenu. Kwa hivyo karibuni muwe watulivu na tushirikiane kuazia mwanzo wa mukutano mpaka mwisho. Chief njoo utuambiye watu wako ili tuanze mukutano mara moja. Karibu Chief. Kamati wako hawako tukaribishe basi tuendele.

**Anasbis Ambari** - Kwa jina mimi naitwa Anasbis Ambari, Chief, Kipini Location, karibuni ma Commissioners, bwana DO hayuko sasa hapa namwakilisha Bwana DO. Kwa bahati mbaya ma Chief wengine wamekuja hivi sasa hawaja wasili lakini wakifika pia muta wajua. Chief Kilelengwani, Chief Ozi. Ma Chief wengine ni kama wa Chara wako mbalo kwa mawasiliano. Leo ni siki muhimu wa hapa Wananchi wote kutowa Katiba ya Kenya kwa sababu Katiba ya Kenya ina kuhitaji wewe Mwanichi mujisikie huru na ma Commisioners nyote hapa karibuni, Kipini yenu hapa. Mujisikie huru hapa katika Kipini Division. Asante ni sana.

**Speaker –** Haya, makofi ni ya kuomba.

**Bw. Omar –** Asante sana Bw. Chief. Sasa ningependa Kamati yetu ya sehemu ya mwakilishi Bungeni Garsen. Kama mujuavio, Commissioner Dr. Maranga, tuko na Constituencies tatu. Pande wa North tuko na Bura Constituency, Central tuko na Galole Constituency, hata hapa tulipo ni Garsen Constituency na hii ndiyo sehemu ya pande ya kusini kabisa na Wananchi wa hapa hawangeweza kufika kwa kikao cha Garsen kwa hivyo nafikiri nitakua tutakuwa tumewaanda mukutano hapa ili waweze kufikia kutoa maoni yao, kwa hivyo naomba Kamati ya wakilishi Bungeni, muje hapa mbele niwataje majina yenu, wananchi awajue na ma Commissioners pia wawajue. Karibuni na mufanye haraka haraka kidogo maana tumechelewa Simame ni hapa.

Basi ma Commissioner, Dr. Maranga, hawa ni badhi ya wanachama wa sehemu ya wakilishi Bungeni ya Garsen. Tuko na Muhamud Gabo, ambaye ndiyo huyu. Tuko na Saidi Rowa, tuko na Mama Hadija Kezie, alafu huyu ni mwakilishi wa County Council ya Tana River, anaitwa Erastus Buko. Tumekuja pia na Chairlady, Mwenye Kiti wa akina mama Maendeleo ya Wanawake Tana River, Mama Sera Wanze. Lakini nafikiri ameenda kusanya akina mama huko. Wana chama wengine ambawo hawako katika Kamiti yetu ni, Area MP, Mbunge wa Garsen Mheshima Molu Shambaro. Tuko na yule ambaye anawakilisha wasiojiweza, Abdulrahman Gobu ambaye hakuweza kufika. Tuko na Muhamud Galole, pia naye hakuweza kufika. Mimi pia Co-ordinator ni member wa Kamati hii ya sehemu ya wakilishi Bungeni. Kwa hivyo munaweza kuketi. Ningependa kwa dakika moja kuwajulisha kwa Area Councillor, naye ambaye tuko naye kwa kikao cha leo, Bwana Yahya. Huyu ndiyo Diwani wa Location hii ya Kipini, na naona ameweza kufika. Tuko na madiwani kutoka, Ozi, kutoka Kilelengwani na kutoka hapa. Lakini hawa sija waona. Kwa hivyo ningependa sasa bila kupoteza wakati zaidi, kurudisha usukani kwenu ili

muelezee Wananchi vile ambavyo watatoa maoni na nimewaomba wananchi kwamba wawe wavumilivu ili tuanze mukutano vizuri mpaka tumalize vizuri. Muko tayari?

**Wananchi** - Answer – Ndiyo tuko tayari.

**Bw. Dhadho** - Asanta.

**Com. Maranga** – Asante Bw. Omar, ambaye ni Co-ordinator. Mimi kwa niaba ya Tume ya kurekebisha Katiba, hii sasa ni mkutano wa Tume ya kurekebisha Katiba na mukutano sasa tutaanza hivi sasa ili tuweze tukasikiza maoni ya wananchi ya uwakilishi Bungeni Garsen. Kwa hivo sisi kama ma Commissioners kutoka Tume ya kurekebisha Katiba, sisi hatuna maneno mengi. Tunataka tu mutuambiye maoni yenu na tutawambia tu mashariti machache ambayo kila mtu ata fuata. Na kwanza kabisa kila mtu ata pewa dakika tano ya kuongea. Utatoa maoni yako kwa dakika tano. Wale ambawo wako na Nakala mameandika, ama Memorandum, unaweza kama utaki kuzungumuzia, unaweza uka kuja hapa ukafanya register, kuna ile register yetu ya official ama rasmi kabisa ya Tume ya kurekebisha katiba, uta jiandikisha na utupe hiyo Memorandum yako. Hiyo ni njia moja.

Njia ya pili, unaweza ukatutolea tu ile maoni muhimu ambayo ume andika kwa Memorandum kwa dakika tano. Kwa hivyo mimi kama Mwenye Kiti wa mukutano wa leo, mimi nitakupa tu dakika tano. Kwa hivyo ukikuja hapa uwe na maoni sawa kabisa. Kama unasungumuzia jambo lolote, kwa ufupi kabisa na kwa ufasaa kabisa ili tuweze. Sisi kama Tume tutayachukuia yale manane. Na ukianza kutoa maoni, ni lazima ujitambulishe kwa majina yako kabisa. Kama mimi ni Fulani, una sema mimi ni fulani, Fulani, alafu hio jina tunataka kuchukua kwa sababu sisi kama Tume, tuna nasa kila kitu ambaye watu wanazugumuza, ili tukifika Nairobi, tuweze tukaona watu wa Kipini walizungumuza nini. Na ni nani alitoa maoni gani? Tunaelewana? Tunaelewana hayo? Kwa hivyo sasa na ile watu ambawo wanataka kuongea, kuna orodha hapa tuna fuata. Unatakiwa ujuandikishe ili tuwe tunajua unataka kuongea. Kama utaki kuongea, unataka kisikiza, vile vile ni sawa. Tunaelewana? Tunaelewana? Tunaelewana? Basi sasa mimi niki kaa hivi, nita anza kuita mtu wa kwanza ili atoe maoni na ukianza kutowa maoni una anza na jina lako kwanza. Tunaelewana? Na akina mama vile vile muna ambiwa muje hapa mbele mutoe maoni yenu kwa Tume. Hakuna mtu ambaye ata piga nyinyi hapa leo. Tume ina waangalia akina mama, watu wasiojiweza. Kuna watu ambawo wasiojiweza kwa mfwano. Kwa mfano wale watu ambawo hawasikii. Tunayo? Wakiija, inatakiwa ni muhimu sisi tuwe tunajua,. kwa sababu tuna yule ambayo anaweza akawasaidia. Waka elewa ni nini tunaongea. Tunaelewena? Kwa hivyo bila kupoteza wakati, wacha niite mtu wa kwanza kabisa, anaitwa Maro Abdul Juma. Keti hapo. Na usungumuze kwa sauti. Una dakika tano Maro.

**Maro Abdul Juma**

Kwa jina langu ninaitwa Maro Abdul Juma, na ni mmoja wapo wa disabled ambawo hawaoni vizuri katika hapa Tana River in Kipini Location. Nimaoni yangu ni section tatu kwa upande wa Elimu na upande wa Ardhi na upande wa Afya.

Upande wa elimu tuna sikitaka sana kwa upande wa disabled hasa upande wa vipofu, tunakuta kwamba Secondary ni moja na mashule ni mengi ya Primaries na hiyo Secondary moja tunakuta kwamba watu ambawo wanaona wanachanganyiwa hapo na kuwasababisha vipofu wengine kukusanyika vijini na kutafuta misaada na ikiwa wanaoona wameungano hapo kujaza shule, hawo ambawo hawaoni, wale ambawo wamepita mitiani yawo kupita points hamsini, points sitini yakuwa wamebakia nyuma sababu nafasi ya Secondary kuwa ime jaa. Kwa upande wa elimu.

Na kwa upande wa Afya. Tuna sikitika sana ya kwamba masipitali zamani hatulipi na ikawa hali ya magonjwa yame zidi Serikali imezidi kuyaweza. Lakini kwa muda huu wa sasa, ikawa Serikali imetoa idhini ya kulipwa pesa na ikawa vifo ni vingi katika humu nchini sababu ya umasikini, watu hawajimudu kulipa pesa.

Na section ya Ardhi. Ardhi kwa hakika, mutu ana uwezo wa kuishi pali popote. Katiba wa umoja wapo ipo. Lakini ni kwamba Katiba hii ina amurisha ama ina zidisha uhalifu. Wa halifu wame kua wengi waki zuka huku na kule kwa silaha ama kutumia hali ya kutumia mdomo kutanisha wananchi. Una kuta wazee wengine ama kwa mfano, watu wengine wanatoka upande wa Eastern ama kwa mfano upande wa Central, ama kwa mfano mutu ametoka Mombasa, anaja aishi area ya Tana River ama Kipini, ana pewa u Headman ama uongozi wowote. Akipata nafasi ya kuuza Ardhi hio na kustababisha vita vya wenyeweye kwa wenyewe. Kwa hivo ninaomba kwa upande huo Serikali, kwa upande wa Ardhi, ione upande huo.

Na upande wingine ambawo ningependa sana kuhimiza ni upande hasa wa shule vile vile. Upande wa shule nikwamba Primaries kunalipwa pesa za building fund, ambazo building hizo kutoka mimi nianze kusoma kwa mfano, tunakuta shule ikiwa niya udongo na makuti, kwa vile vile na pesa hizo zinatolewa nyingi. Kwa hivo inaonekana pesa hizo zinatumiwa kimafluki. Kwa hivo sisi tuwanainchi kwa niaba yawo tunaomba pesa kama hizo zitolewe. Nime malizia hapa kwa ufupi mimi. Asante.

**Com. Maranga**

Tunaomba ngojea subiri kidogo. O.k. ujiandikishe kitabu chetu rasmi hapa na asantesana tunashukuru sana kwa maoni yako. Mwingine anaye fuata ni Councillor Yahya Shabir.

**Cllr. Yahya Shabir**

Mimi jina langu naitwa Yahya Shabir Bwana Mahazi, Councillor wa hapa Kipini. ambapo saa hii tupo. Maoni yangu mimi kuhusu marekebisho ya Katiba. Kitu cha kwanza katika Katiba yetu ya mbele au Katiba ambayo saa hii tunatumia, hakuna jina la Mwenyezi Mungu katika Katiba hio. Kwa hivo maoni ya kwanza ni kusema Katiba hiyo ya sasa iwe na jina la Mungu nalo liseme hivi. Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mfalme wa Wafalme. Hayo ndiyo maoni yangu kwanza katika Katiba hiyo.

Na kitu chengine, katika Katiba hio ya sasa tunataka, kuna shida kubwa ambayo inatupata sisi wenyeji wa Kipini kuhusu habari ya Ardhi. Area ya Kipini ama katika Ardhi, Ardhi ime gawanywa katika sehemu mbili au tatu. Kuna sehemu ya kwanza ambayo ni Trustland na kuna sehemu ya pili ambayo ni Crownland na sehemu ya tatu ambayo ni Title Deed. Lakini Area ya Kipini ni sehemu ambayo ni Crownland. Crownland inatolewe na Commissioner of Lands ambapo Commissioner of Lands anaweza toa Ardhi hiyo bila ya kufahamu kwamba hapa Kipini, kwamba hapo pana shamba kwahivo maoni yangu ni kwamba Ardhi ya Crownland iwe chini ya Chief pamoja na Wazee ndiyo waweze kupeyana Ardhi kama hiyo. Isiwe chini ya Commissioner of Lands, kwa sababu inapo kuwa chini ya Commissioner of Lands, Commissioner of Lands ajui mambo yale ya Kipini.

Na vile vile nikiongezea jambo hilo, madhumuni ya kusema neno hilo kwamba Commissioner of Lands asipeyane Ardhi ya Crownland, kwa sababu mbili. Sababu ya kwanza, hapa Kipini, kulipeyanwa Ardhi ambayo ni ya Beach Plot ilipeyanwa huko Nairobi. Ambapo wenyeji wasehemu hii hawakuweza kupata Ardhi ile. Watu waliochukuwa Ardhi ni wale walioenda Nairobi, wakaweza kutengeneza makatasi, watu wa Kipini wasiweze kupata zile Letter of Allotment. Kwa sababu Letter of Allotment zili toka mfano nikama Letter of Allotment alufu moja watu wa Kipini waliopata nikame watu thelathini. Hiyo nikusema nikama watu wa Kipini hawakupata kwa sababu ilitolewa Nairobi.

Na kitu chengine, kuna Ranch hapa inaitwa Nairobi Ranch. Ambayo Nairobi Ranch ni ya mutu amemeliki ako na Title Deed. Na katika Ranch hiyo kuna njia ya kupita kwenda Mpeketoni ambapo wenyeji wa sehemu hii wanapo tumia njia hiyo, wanapo patikana na wenye hiyo Ranch, wanachukua baisikili wana weka puncture, na yule mwenye baisiki wana kata kabisa hiyo gurudumu, yule mtu anabakiya hana namna ya kubeba, kwa sababu ile Ardhi ameimiliki kwa njia ya Nairobi. Lakini kama ingekuwa hiyo Ardhi imeamelikia kwa njia ya kienyeji, basi wasingeweza kumeamiliki namna ile kwa sababu ile barabara inge tambulikana.

Na jambo jingine hapo hapo tukienda kwenye Ardhi, kuna Ardhi ambazo zina kuwa zinatolewa kwa Nairobi, ambazo Ardhi ile itakuwa kuna slaughter pale ndani bila ya Commissioner kujuwa. Itakuwa ile Ardhi kwamba pana mutu ile Ardhi ita peyanwa kwa mtu. Na vile vile kulingana na marekebisho haya tunaya taka kwamba squarters anajulikana kuwa ni squarter, baada ya kuishi pale mahali kwa miaka kumi. Sasa marekebisho tunataka squarter ajulikane pale baada ya miaka miwili peke yake.

Kuhusu jambo jingine ambayo tutaondokea kwenye Ardhi, ni kuhusu mambo ya Troller ambayo kuna meli ambayo ina buruta samaki hapo ambayo ni ma Troller, ambayo serikali ina benefit kuhusu hizo Troller, lakini mwanachi wa Kipini hapati kitu chochote kwa hizo Troller na Troller hizo zina chukua samaki na inapata pesa nyingi sana, ambayo mwananchi wa hapa yeye hawezi kunofaika na Troller hiyo iko kwao. Ni maoni yangu kwamba, nusu ya yale mapato ambayo yatapatikana kwenye wenye ma Troller yawe inagawanywa kwa wananchi.

Na wakati huwo huwo, ikiwa kwamba kuna mapato baada ya hiyo kwa wananchi, na vile vile Troller isi ruhusiwe kisheria iwe itavua kwa maeli mbili na nusu baharini, maili mbili na nusu.. Ile maeli mbili na nusu ambayo itakua sehemu hii ya uvuo ambapo itakua ni ya wenyeji na Troller ikitaka kuingia sehemu hio, isiweze kupata nafasi mpaka waone wenyeji waweze kuwakubalia au wakatalie.

Jambo langu jingine la mwisho ni kuhusu mamlaka ya Baba wa Taifa. Baba wa Taifa, kitu cha kwanza ninasema asiwe above the Law. Asiwe juu ya sheria, awe chini ya Sheria. Na asiwe na mamlaka ya kuchagua moja kwa moja mawaziri na ma PS's wake. Yeye anapendekeza, anapeleka kwa Bunge, na Bunge ndiyo liamuwe kwamba fulani anafaa kuwa waziri, apigiwe kura, kama vile ma Councillors wanavyo pigiyana ma kura au kumchaguwa Mayor. Na mawaziri wawe hivyo. Na yule waziri ambaye atasimamiya Ministry inayo husika, kwa mfano ni Health, lazima yeye awe Daktati, anaejua mambo ya afya. Na yule Mwaziri ambayo atasimamia mambo ya mfano Education, lazima angalawo awe na Degree ya Masters, ndiyo aweze kusimamia hiyo.

Na mwisho, Bw. Commissioner, nakwambia, kwa ma Councillor, mapendekezo yangu, Councillor asiruhusiwe kusimama ikiwa Councillor huyo angalawo hatakuwa na elimu ya shule ya msingi, chetu cha msingi.

**Com. Maranga**

Councillor ujiandikishe hapo. Asante nashukuru kwa maoni yako. Mwingine ambayo anaefuata ni Islam Abdalla. Islam Abdalla. Ako? O.K. Sawa.

**Islam Abdalla**

Mimi ni Islam Abdala, Chairman ya Kanu ya hapa Kipini. Maoni yangu kuhusu marekebisho ya Katiba

**Com. Maranga**

Tafadhalini mukaye kimya. Patieni Islam Abdala wakati.

**Islam Abdalla** – Maoni yangu kuhusu marekebisho ya Katiba. Kitu ya kwanza ambayo nimeweka number one, nikuhusu Sheria ya Ardhi katika Kenya. Hii Sheria kulingana na utalam ambawo tuko nawo, haitusaidi sisi kama wananchi wa chini. Hii sheria ili ridhiwa kutoka kwa wakoloni na ni sheria hii ambae ime wanya wale watu ambawo wako juu wamalize hizi Ardthi za wananchi. Kwa hiyo hiyo sheria aifai kuwekwe sheria ambayo inatokana na wananchi.

Kitu ya pili, ni kuhusiana na mali ya asili. Kwa mfano kama mali ambayo iko baharini, iwekwe sheria katika Katiba hii mali hiyo isichumwe na watu kotoka inje ya sehemu hii. Kwa sababu, mfano kama mwezangu ametoa, tuna meli za uvuvi ambawo zina chukua pesa mingi, resources nyingi yetu inaenda na wawo na sisi atufaidi kitu. Tumebaki katika umasikini, ma shule zetu zime haribika, kila kitu yetu ni mbovu, afya zetu zimekua mbovu na vile hali inchi yetu ni tajiri.

Neno pengine itakua ya mwisho kwa sababu sitaki kuchukua wakati wa watu wengine, ni kuhusiana na huduma za afya. Huduma za afya kwa wakati huu, ambazo ziko katika Katiba yetu, hazi tufai kabisa. Kwa sababu masikini wanaumia. Kama huna ule wanaita Cost sharing ndiyo wame lete zusi, basi wewe uwezi ukatibiwa. Kwa hiyo tunataka huduma za afya ziwe bure. Zisiwe za pesa. Kuna watu wengine hawezi kumilika hata shilingi mia moja. Kwa hiyo iki fika ni hali ya ugonjwa, yeye atapata shida sana.

Pengine, nafikiri ingine ambayo ninge jaliza hapo kidogo ni kuhusu hii uwezo ambayo iko ya utawala. Uwezo ya utawala ya nchi isiwachwe mikononi kwa mtu moja. Kwa sababu kulingana na vitabu tume soma soma kidogo, tumeone uwezo wa ukuu wa nchi iko kwa mtu moja. Kwa mfano kama nchi na nchi inataka kupigana, mutu moja akiweka kidole, basi wananchi ambawo hawana hatia, wataenda kuangamia. Tunaomba sheria hii ibadilishwe na uwezo kama huwo ipewe Bunge ndiyo waweze kuamua. Sina zaidi. Asanteni.

**Com. Maranga** – Asante Mzee Isam. Asante kabisa. Jiandikishe maoni yako tumeya pata kwa uzuri kabisa. Anaye fuata ni Awadhi Mubarack. Awadhi Mubarack? Haya, karibu. Haya una dakika tano.

**Awadhi Mubarak** – Jina langu ninaitwa Awadhi Mubarak Hassan na ni Organizing Secretary wa Kipini Fisherman Association. Maoni yangu ni kwamba faida zinazo toka kwa mali ya hasili, inufaishe jamii yenye mali asili hiyo.

Lingine ni kwamba mukagusi mkuu wa fedha za uma, achaguliwe na wananchi. Mali ya asili kama bahari na vilizomo, miti, misitu ziwekwe chini ya usumamizi wa wananchi wenyewe. Na mali asili hizi, zilindwe kutokana na uharibifu.

Kuwe na mugawanyo wa uongozi. Tuwe na Prime Minister. Tuwe na kila jimbo kuwe na Chief Minister. Maafisa wa Uma pia ni lazima watangaze mali yawo tuweze kuyajuwa.

Tarehe ya uchaguzi iitwaje moja kwa moja kwenye Katiba hii tunayo tengeza. Kama kiongozi ni miaka minne twajua ni mnne

sie Prime Minister ama ni miaka mitatu, tujuwe ni miaka mitatu.

Na Prime Minister achaguliwe moja kwa moja kutokana na wananchi. Alafu Chief Minister, achaguliwe na wananchi. Chief Minister ndiyo atamchaguwa Prime Minister katika zile sehemu zao wanazo wakilisha. Kuwe na Prime Minsiter kila Mkoa.

Commissioner ya Ardhi. Commissioner of Lands asiwe na uwezo wa kutoa Ardhi kabla haja aja moja kwa moja kwa wananchi. Kuundwe Tume ambayo itakuwa na uwezo wa kugawanya zile Ardhi kwa Commissioner of Lands, mwanzo anakuja kwa wale, ile Baraza la wazee. Anauliza je, bwana fulani anafaa kupawa Ardhi? Ndiyo Commissioner of Lands ana issue. Ikiwa hakupatiwa kutoka kwa wazee, basi Commissioner wa Lands asiwe na uwezo wa kupatiana Ardhi ile.

Hawa wavuvi wakubwa wanao tajwa ambawo wezangu wasa taja kabla, wasi weze kupawa leseni na wavuvi wowote wale ambawo ni wakubwa wakubwa wanaweza kudhulumu wadogo, wasi pewe leseni kabla hawaja ruhusiwa na wenyewe wenye mali yawo. Kwa hivyo kama ni Director wa Fisheries ndiyo anatoa leseni, amwambiye ule mvivu mkubwa kafanye makubaliano, uniletee makubaliano ndiyo nimpee leseni. Kwa uchache ni hayo. Asante ni sana.

**Com. Maranga –** Karibu. Keti tu. Pengine unaulizwa maswali. Na mimi sina swali. Lakini weka sahihi. Weka sahihi Asante kwa maoni yako lakini. Next anaitwa Salim Hiribai. Salim?

**Salim Ali Hiribai –** Kwanza Asalamaleikum.

**Wananchi –** Aleikumsalam

**Salim Ali Hiribai** - Jina langu naitwa Salim Ali Hiribai. Kitu cha kwanza ambacho twataka tukizungumuze hapa kwenye Tume hii ya Katiba, ni kulingamana na elimu ya skuli. Elimu ya skuli, watu wote ambawo tunasoma, wengine wana nguvu, wengine wana afya, wengine hawana, twaiomba serikali ikiwa hii ya Tume ya Katiba, ikiwa yawezekana, basi mtu akianza Primary mpaka Secondary mpaka University - bure.

Kitu cha pili ambacho twataka kukiomba kwa Tume hii ya Katiba, ni kulingamana na mto ya Tana River. Mto wa Tana River umekufa. Na sababu ya kufa wa mto wa Tana River, ni kusema huko kumekwa mabawa nasisi mabawa yale haya tunafuishi katika huku watu ambawo wameathirika. Chumvi unaojaa kwetu huku mtoni. Inaojaa baharini upande wa mpaka mashamba. Twaiomba Tume ya Katiba iwapo yawezekana, wale wanaolima pande hizo au wale wanaothirika pande hizo, wapawe msada kwa kila miezi mitatu, yale mapato inaopatikana, na wawo wapate. Wale walioathirika.

Kitu cha tatu. Twa omba Tume ya Katiba kulingamana na Title Deeds. Sisi hatuna Title Deeds umu mwetu. Title Deeds ni mashamba ambawo yakutoka mababu na mababu. Basi ikiwa yawezekana hayo, hayo mashamba ya mababu, nasisi tuweke

Banki, tuyapeleke Banki kwamba hii shamba hii yajulikana na Chief, yajulikana na DO, yajulikana na fulani kwamba shamba hii ni ya fulani. Na mtu alipeleke Banki apate pesa kama wale wanavyo pata pesa, wale ambawo wana ma Title Deed.

Kitu cha nne. Ni kusema hali ya matibabu yame zungumuzwa sana. Na mimi nataka kuyaongezeya. Hali ya matibabu. Watu wa wahudumiwe sipitali kutoka hapo sipitali hii mpaka ya Kenyatta, mpaka hadi mtu aende akapowe bila kutowa peni.

Twaiomba serikali ya Tume ya Katiba hala ni Tana River ime umia kwa hivyo twaitaka hala ifanye bidii ale kuli hali itupe Title Deed na sisi tuitumiye Tana River hii. Twaiomba Tume ya Katiba badala ya kutumia hii - twaiomba Tume ya Katiba itusaidie wale wazee ambawo wamekua wakongwe, kwa sababu apawa mtu mshahara million nzima mtu moja na huku kuna wazee ambawo wana miaka sabini, themanini, wafaa na mayatima wafaa. Tuaiomba serikali au Tume ya Katiba iwape fidhia wale wazee wasiojiweza awasaidie. Nafikiri yangu hapo yatosha.

**Com. Maranga –** Asante Mzee Salim. Tume inakuomba tu uweke sahihi. Hiyo utupatie uandikishe hapa. Enda pande hiyo ingine. Tunashukuru sana. Kabla sijaita mwingine, pengine ningewajulisha, Commissioner mwingine amefika ambaye amekua amechelewa kidogo kwa sababu alikuwa na hitilafu kidogo hapo Malindi, anaitwa Com. Alice Yano. Ebu salimia watu wa Kipini.

**Com. Alice Yano –** Hamjamboni nyote. Asante.

**Com. Maranga –** Huyo anaitwa Com. Alice Yano. Ni mmoja wa Commissioner wa Tume ya kurekebisha Katiba. Sasa tumuite Matiko Mulatia. Matiko Mulatia?

**Matiko Mlatia –** Kwa jumla habari zenu? Mimi naitwa Matiko Mulatia wa hapa Kipini Division, Location Matangeni, Shauri Moyo Village. Sasa mimi naona hapa tuko kwa kutengeza Katiba. Lakini na shangaa sana kuona mutu ameajiriwa hata kama anatumwa na askari na hakuna malipo. Sasa hapa tulifanya kukusanywa na Chief. Aka tuma ma barua tupeleke ma Headmen. Headmen hakulala kutoka juzi mpaka leo. Na hakuna malipo kabisa. Na anafanya usiku na mchana. Huyu mutu hata sijui ni wa roho gani. Hata ajui kudai. Sasa tunaomba kwanza Headmen alipwe na serikali. Sababu ana nyimwa na family yake. Na serikali ile iko kutoka hapo kwa Headmen mpaka kwa Moi, inanza kwa Headmen, kwa nini alipwi. Na walimu wa Primary wanalipwa. Nursery wanalipwa. Huyu kwanza apatiwe malipo. Sisi hatuko tiyari kufanyiwa kazi na mtu ambaye alipwi. Hiyo ni kama kunyanyaswa Mtu anatumiwa kama mbwa. Kama ni mtu ambaye hana akili yake. Lakini anajitowa tu. Alipwe. La sivyo atolewe kwa hiyo. Tuwe hakuna Headmen. Akaye apumuzike. Sababu anafanya kazi bure hiyo. Hiyo ni moja.

Pili. Turudi kwa Elimu. Elimu afadhali hiyo Ministry iwawe kabisa. Sababu wakati wa budget, kweli ina pangwa na ina somwa vizuri mwezi wa saba. Tukiangalia hiyo Ministry inagawa pesa. Na mzazi anawachiwa kazi. Vitabu, matibabu hata ya shule na nini,.watu ya mbao. Viti vya kikalia. Shule ni yeye. Hiyo pesa na tunaona wanapangiwa budget, inaenda wapi? Na mzazi

ndiyo ana towa pesa. Na aipatikani. Kwa hivyo hiyo Ministry kama usaidizi hakuna iharibiwe huko ata isi tajwe huko. Isitajwe kabisa. Tubaki bila. Muzazi ajitegemee.

Haya. Sasa ni kuhusu wakati wa zamani. Wakati kwanza wahapa, wakati wa Kenyatta tukilenganisha. Kwanza mimi nina uchungu mingi sana. Mimi Matiko. Kusikia watu wali kufa ovio ovio Nairobi sababu ya kunyimwa haki zao. Sababu ya ile pombe ya ten ten. Mutu, matajiri wote wamejengewa magorofa ya bar. Sisi wengine natumia pombe sisi, bila kuficha. Lakini, ile kidogo napata unafungua brake kabisa hata ki vilabu zile za zamani hakuna. Na ulevi ni ule ule. Sasa naye mwenye kutengeza pombe hii usiku hapeyani kwake. Mtoto amependa kwenda Secondary. Ame pita. Sasa anatafuta atengeze pombe kali. Na mtu ya kusimamia ile chemicals hakuna. Sababu ana tengeza kisiri. Polisi ataki wajue. Na municipal ile ilikuwa inapima pombe wakati wa vilabu hakuna.

Sasa huyu anatengeza kwa sababu shida, sababu mtoto amepita. Haya mwenye kunywa naye anakunywa kiuizi. Sababu hataki ajulikana. Na pesa kwenda bar hakuna. Kwa hivyo ni kumanisha wakubwa, wakubwa wame tengeze starehe zao, sisi raia tuna umia. Hata ukipata namawazo, uwezi kupata chupa moja. Ukienda bar, huna uwezo. Na huku polisi wanakungojea. Siku ya ten, ten hakuna mutu mukubwa alikufa siku hio. Masikini ndiyo walikufa bara barani sababu ya kukunywa pombe haramu. Sababu hawasimiwi na serikali na ma daktari wakiwekewa. Kwa hivyo hizo vilabu vya starehe za zamani tupewe. Hakuna mutu hana shida. Anataka kuburudika kidogo kama wakubwa. Hawatushindi raha. Ni vile hatuna uwezo wa kwenda huko.

Kuhusu mukulima. Sisi natumiwa tu, natumana pande zote. Serikali inatuwachia mukulima na mteja. Na hapa kati kati mali kutoa kwa mukulima, kumpeleka kwa ule mteja, mteja ako peke yake. Na ninge shika brake nikama pamba nauza na shilingi ishirini niki hesabu ile garama ya dawa na kila kitu, imeanguka. Haya, nimeuza pamba jana na huyu naye atembeya na gari. Nguvu ni zangu. Namomba lift. Hata anaweza kunipata bara bara, na mali ni yangu. Serikali ile, ni ile tutaunda leo, na Katiba vile tutaunda, isimamie mali ya mukulima kukatisha kunyanyaswa. Na tu market tutafutiwe. Hapa staki, huyu ni tajiri, na hapa kuna brokers. Sija sikia mali yangu kuwekwa brokers kati kati. Nikutoka kwangu direct kwa tu sikizane. Na Katiba ile itaundwa isimamie mukulima afaidike. Sina mengi.

**Com. Maranga –** Asante Mzee Mlatia. Haya jaza kitabu yetu. Yule anayefuata anaitwa Ngala Insano. Ngala Insano? Haya.

**Ngala Insano –** Habari zenu nyote? Asanteni kupata nafasi hii kwanza. Ile ninataka kuchangia kwa Katiba hii yetu ya Kenya ni kwamba katika sehemu za mashamba, hatuoni usalama wa kutosha. Ilo ni la kwanza. Kwa sababu huduma wowote tunaone umekaa kwenya miji. Tunaiomba hii marekebisho ya katiba iweze kuangalia vizuri kuhusu watu wana kaa kule mashambani. Kwa sababu hakuna police, KPR hakuna, Game hakuna, ni wale jamii tu wanaishi kule. Hakuna sasa wana kaa kule kuomba Mugu tu. Hali mijini wakilindwa vizuri. Hilo ni la kwanza.

Na kitu kingine ni kuhusu Police na huduma zao. Polisi kama siku wachochea, nina jaribu kuwakosea kidogo kwa sababu wanaonea watu sana wa mashamba. Una kuta polisi wanakuja kwa mashamba wanakusanya watu, bila kujulisha hata Headmen huko. Wanasumbua watu baada ya kwamba wawe msaada kwa watu, wanakua vitisho kwa watu. Tunaomba urekebishaji huu wa Katiba uangalie sana jambo hilo.

Na kitu kingine ni upande wa elimu pia. Elimu, wakati tukiwa tunajaribu kungangana na ujenzi, tunaona kwamba hatuna msaada wa administration. Hivyo ni kusema pengine Chief, DO na hata Assistant Chief wakati mwingi, ujenzi wetu huwa tunajaribu kuvutana vutana lakini office ndiyo nguzo yetu, ndiyo inaotusukuma ama kutufanya tuweze vizuri. Lakini tunaona nguvu zao hawa ma Chief wetu zina rudi chini sana. Na hivyo tuna vifiya. Tunaona kulingana na urekebishaji pia hawa ma Chief wawe watu wa kuongoza mbele kuhusu mambo ya elimu, hivyo nikiongezea hapo elimu pia iwe itakuwa ya bure kidogo kutoka Nursery mpaka ikiwezekana hata Form Four. Kwa sababu tunaona kwamba ni wengi wenye kuenda mpaka Form Four wale wenye uwezo, hasa hawa wasio na uwezo watoto wao wanapita mitihani lakini wasiweze kuenda kule, Kwa hivyo serikali ichukuwe hatua hiyo yaku wasaidia watoto kama hawo waweze kusoma kama wale wenye uwezo. Nime horodhesha mambo mengi sana lakini hayo machache.

**Com Maranga –** Nashukuru hiyo Memorandum yako inatakiwa ujiandikishe hapa na asante sana nashukuru kwa maoni yako. Akina mama namna gani. Nyinyi hamtaki kutoa maoni? Akina mama wale wanataka kutowa maoni wajiandikishe vile vile. Sasa namwita Issa Kinaushuru. O.K.

**Issa Kinaushuru Ndilo –** Mimi naitwa Issa Kinaushuru Ndilo jina langu yenyewe hilo. Kwa hivyo kuchangia hii maoni ya Katiba, kwanza ningependelea hivi. kila moja arudishiwe haki yake. Sababu kulingamana na kusema hivyo, una kuta mtu yuko ngazi za juu huko anamnyanyasha huyu wa chini. Kwa hivyo mimi ningependelea kila moja arudishiwe haki yake. Kama hawa wanapokuwa wanagawanya hii Ardhi, uwa wanagawanya ile gazi za juu, hawa wa chini hawajui. Alafu wanafanya kama a squarter. Alafu yeye huwa hana nguvu. Kwa hio inabidii haraka sana aondoshwe. Kwa hivyo, kila moja awe amerudishiwe haki yake na amepatiwa haki yake sawa sawa.

Jambo ya pili, hi Tume ya Katiba iwe iko na jina la Mwenyezi Mungu. Iwe imewekwa hapo kwa jina la Mwenyezi Mungu alafu Katiba iwe inaendelea.

Jambo la tatu. Mukulima na Mfugaji wawe wamewekwa mbali mbali. Sababu ikiwa wamechanganywa pahali pamoja, uwa inaondosha vita. Inaleta hasama hiyo.

Na jambo lingine, nikusema hii nguvu ya serikali, iwe imegawanywa kwa kila mwanachi awe amepatiwa. Wawe ma chiefu na ma DO wawe hawana nguvu zile za kumushika mutu kabisa uweke chini ile imetokana na ma sub-Location Ndiyo alafu ndiyo wapelekewe nguvu. Sio nguvu kuchukuwa mikononi kwao.

Na huu President mwenyewe wa kutawala nchi, awe sio kama amechukuwa funguo za silaha awe ni yeye pekee yake. Awe ameshika, yani apunguzwe zile nguvu ambazo alikuwa yuko nazo. Kwa hio awe amegawanyiwa yale madaraka ya gawanywe kila mtu apate, zile haki. Ndiyo sababu kusema kila moja amepatiwa haki yake.

Kwa hivyo, na haya masomo. Masomo yawe yametolewa bure. Sababu kuna watu wana pesa nyingi. Kuna wengine hawana pesa na wako na tama ya kusomesha. Inakua yuko na tama ya kusomesha na hana ule uwezo ya kusomesha ina bidi anakosa masomo. Kwa hivyo ningependelea hii Katiba tunaotunga hivi leo wawe wa serikali wako na pesa nyingi sana serikali wanachukua alafu wawo wenyewe huwa wanajibanisha tu hawo wenyewe, hawa masikini hawaangaliwi. Na masikini ni wengi kuliko wale matajari. Sio kama wawo ndiyo wawo peke yawo. Na Mwenyezi Mungu pia hawa masikini amewaumba yeye mwenyewe kwa hivyo ana wajua. Na yeye amewekwa nikiongozi ana wanyanyasa hawa wote walioko huku chini. Kwa hivyo hii Katiba napenda mimi kila haki ya mmoja iwe ime rudishwa kwa mwenyewe – ewe mwananchi.

**Com. Maranga** – Asante Issa

**Sera Wande** - Mimi kwa jina naitwa Sera Wande, kiongozi ya wakina mama katika Wilaya hii. Yangu si mengi. Vile ni mama nina machache ambayo ningeya zungumuza ili Katiba iangaliwe na sheria ziwekwe kuhusiana kwanza kunajisiwa musichana bikra. Tume amua kwamba mutu kama huyo afungwe kifungo mara mbili ya ile sheria ilioko sasa ya miaka saba.

Kitu ya pili, kama ni baba kwa mtoto, yani baba ambaye amemnajisi mtoto wake na anamshawo mama anaendelea na yule msichana walie mzaa na huyo mama, huyo mtu adhibiwe hadi kufa ama sio akatwe, yani ambaye yali mfanya, yali mpleke kwa mtoto kuliko bibi yake akatwe kabisa.

Kitu ya tatu, ni mshahara ya wabunge. Tuli amua kwamba ikiwezekana na iwezekane, wabunge mshahara yawo ipunguzwe, iwapatiwe wale wabunge wa mashinani, yani Councillors ili waweze kusaidiana kisiasa.

Kitu ya nne niliofikiria ya kwamba, ya hali za sheria zilioko kwa ma Kadhi zinasaidia sana. Lakini kwa upande mwingine, zina nyanyasa wa mama, sababu baada yakutoa uamuzi wa Kadhi, hata kama mama ana mambo ambayo yanambidi awezi kupeleka popoto pale, tunauliza serikali iwekwe Katiba kwamba kuwe na a appeal kama yule mama anafikiria anaweza ku appeal iwezekana katika serikali yetu ili mama naye aweze kupata haki zake. Asante sana.

**Com. Maranga** – Asante mama. Tafadhalini tunakuomba uweke sahihi kitabu chetu rasmi na hiyo Memorandum yako. Hiyo ni sawa utuwachie. Enda pande hiyo uweke. Yule anayefuata anaitwa Mwanze Musili. Mwanze Musili? Haya. Nafasi ni yako.

**Mwanze Musili Kakuli** – Kwa jina naitwa Mwanze Musili Kakuli. Natoka hapa Kipini Shauri Moyo. Maoni yangu ya

kwanza ni kuhusu hawa ma officers wa polisi. Maoni yangu ya kwanza ni kuhusu polisi. Utakuta polisi wana nyanyasa hasa sisi wananchi. Polisi unapo mtuma mahali aende kushika majambasi wanatokea, yeye aendi. Una report saa hiyo asubihi, yeye anachukuwa muda anakuja kitu kama saa saba mchana ambayo majambasi wametoroka. Na ikitokea kwamba iko mahali pombe haramu inapikwa, saa hii hata anaweza kwenda kulala mahali pale, ili avamie walevi. Na ili hali kazi yake ya kuvamia majambasi musituni anashindwa nayo. Kwa hivyo hapo tunaomba kikosi ya polisi kirekebishwe, katiba irekebishe hapo.

Nikiendelea kwa upande wa polisi, utakuta hawa ma traffic wanaumiza sana ma drivers. Unaenda unakuta traffic ako pale, mwingine ako pale, na anakuambia toa kitu kidogo. Na gari yako pengine ni mbovu, hata aangali ni nini inaendelea kwa magari, yeye yake tu kukuonyesha chini, mahali ambaye utawachilia pesa chini. Yeye aangali gari. hata ashuguliki hata kama gari yako imetoka saa hii kununua, yeye anakwambia utoe kitu kidogo. Kwa hivyo ma officers wa polisi pande hio tunaomba wajirekebishe sana. Tuangalia Katiba vile itawafanya na ikiwezekana officers wa polisi wanapo ajiriwa kazi asichukuliwe tu. Wengine walikua majambasi, wengine walikua wakora, na anaingizwa katika kikosi ya polisi hana discipline. Kwa hivyo ningeomba Katiba ingalia ikiwezekana hawa ma officers wa polisi waka kaguliwe hata mpaka kwa jamii zawo, hiyo jamii inakaaje ndiyo officers wa polisi aweze kuajiriwe. Kwa maana mwingine utaweza kuajiriwe alikua makanga njiani. Kana kuja kunyanyasi sisi wanachi. Kwa hivyo nina ongea kuhusu hapo kwa polisi.

Jambo ya pili ni kuhusu hawa makanga. Katiba iangalie kweli kama makanga wanaweza kuwa ndiyo ma brokers zetu, maanake unapo simama stage, kwanza unaongea na makanga ndiyo upate kuingia ile gari. Ikiwezekana Katiba iangalie kweli hawa makanga wametoka wapi, nani wakora manake uta ingia gari ile mpaka uonge na makanga ambaye zamani ilikua unangia moja kwa moja kwa gari bila kupitia kwa makanga.

Jambo lingine la tatu langu, ni kihusu haki za wazee. Tume angalia sana tumekuta iko haki ya mtoto, iko ya akina mama. Lakini sisi naye wazee, tuangaliwe sana. Tuwangaliliwe haki zetu. Unakuta mzee kwa mfano ako na mabibi wawili. Huyu bibi wa mwisho amemuoa, mzee ndiyo anampenda zaidi, ako na yeye na anawangalia. Huyu bibi wa kwanza kwa sababu kijane yake ni mkubwa, anachochea kijane yake asimpe hata mzee ndururu. Kwa hivyo sisi wazee, tuangaliwe zaidi, tunaumia jamani. Kwa sababu unakuta mama anakuchochea hata chakula ukuti kwa nyumba. Kwa sababu ya hawa watoto wetu. Mtoto nimemzaa na hanipi ndururu. Kwa sababu ya mama. Kwa nini? Kwa hivyo katiba iangalia ikiwa mzee naye anafaa aangaliwe masilahi yake iko namgani.

Jambo langu la mwisho ni kuhusu ma drivers. Sisi wa Kenya, maisha ya mwanadamu ni za dhamana sana, na inafaa iangaliwe zaidi tusije tukabebwa na ma drivers wengine, ambawo hata hawana tabiya. Unakuta mutu amejifunza gari hapo bara barani tu, hajaenda college yeyote ya udrivers. Ameajulia tu kwanba yeye ni mumakanga. Na anapewa licence. Licence yake amefanya kununua, aendi kuifanyia kazi uvumulivu analipwa pesa pale anapewa leseni na yeye ni mukalaji wa mirra, bangi anavuta ako na ma ruster, na anabeba raia ambaye mwanchi ni mtu ya dhamana sana. Ningeomba Katiba ya sasa iangalia zaidi, irekebishe kuhusu ma drivers. Maisha ya mwanadamu iangaliwe zaidi ibebwe vizuri. Sio kubebwe na mutu ambaye anakula miraa huku,

anavuta bangi huko, kwingine unakuta ana chimney za ma sigara. Tuangalie tafadhali mwananchi abebwe vizuri kama chopo cha dhamadha. Yangu ni hayo.

**Com. Maranga –** Asante Mzee Musili na nakuomba uweke sahihi kitabu chetu rasmi na nimeshukuru sana kwa maoni yako. Anaye fuata anaitwa Wilson Malibe. Wilson?

**Wilson G. Malibe-** Jina langu ni Wilson G. Malibe. Nitaanza na utangulizi wa Katiba ya Kenya. Ianze na wimbo wa Taifa, kwa sababu Mwenyezi Mungu hakutajwa katika Katiba ya kwanza.

Kuhusiana na mambo ya Ardhi, sheria za umulikaji ya Ardhi zirahisishwe zianzie vijijini mpaka kwa Baraza ya Wilaya. Wapewe uwezo katika shuhuli hizo za ugawanyaji wa Ardhi kisheria. Kusiwe na neno Squartter kabisa. Kila mutu atakae pewa Ardhi akaye kwa muda wa miaka mitano au zaidi asiitwe squartter bali awe na haki ya kumiliki ardhi hiyo. Kuwe na Kamati ya ardhi kuanzia vijijini ziwe na uwezo kutoa ardhi hiyo.

Kwa upande wa ulinzi na usalama, kuwe na baraza la usalama litakalo husika na usalama wote ya nchi na viombo vyote vya usalama. KPR wapewe zana za kisasa kupambana na majambasi na kulinda vijiji vyawo na mali zawo.

Katika upande wa mali. Mutu yoyote atakaye pora mali ya uma, mali yake yauzwe na pesa zirudishwe katika serikali.

Neno corruption au kashfa serikalini na kwenye mashirika iondoke na iwekwe sheria kali katika Katiba ya sasa kuhusiana na corruption.

Vyama vya siasa viwe vitatu.

Kwa upande wa mali wa asili, imilikiwe na kuifadhiwa na wananchi wenyewe katika maenewo itakayo patikana.

Kwa upande wa Bunge, wananchi wawe na uwezo wa kumtoa mbunge kwa kura ya kukosa imani naye. Na kuchagua mwingine badala yake hata kabla ya muda wake Bungeni, ikiwa hata waridhisha wananchi hawo.

Katiba ma baraza ya Wilaya, Mayor achaguliwe kwa njia ya kura na wananchi. Na ma Councillor pia, ikiwa hawata tosheleza majukumu yao na kuridhisha wananchi, pia waondolewe kwa kura ya kukosa imani na wachaguliwe wengine kabla ya muda wao. Yangu ni hayo.

**Com. Maranga –** Asante. Asante Bw. Malibe. Utuwekee sahihi katika kitabu chetu rasmi. Nashukuru wewe. Mwingine ambawo tunamuita ni Said Muhamed. Said? Karibu. Una dakika tano.

**Said Muhammed** - Salamaleikum.

**Wananchi** – Aleikumsalam

**Said Muhammed** - Kwa jina naitwa Said Muhammed, nikiwa kama chairman wa Youth Group. Mapendekezo yangu, kwanza ninaanzia kuhusu rasili mali. Rasili mali ndiyo kitu muhimu ambacho tuko nacho, na ni lazima tuifadhi na ni vipi tuta tumia. Napendekeza rasili mali zifadhiwe kimila na desturi za kienyeji. Vedi vya matumizi ya rasili mali zihidhimishwe na jamii inayo kalia sehemu hizo,
Ushuru inakosanywa kutokana na rasili mali za sehemu hizo utumikie jamii na miradi ya uma.

Vyeti inaingilia upande wa ardhi. Vyeti vya kumiliki ardhi vitolowe na jamii ya sehemu hiyo iwe ni kuongoza, kushuhulikia, vyeti vya kumiliki vitolewe na wenye ardhi. Serikali iwe ni kuongoza na kushuhulikia utaratibu unaotakikana.Tuwe na mahakama ya KiIslamu, ambayo itatumia sheria za KiIslamu. Na wachaguliwe na Waislamu. Nimefikia hapo.

**Com. Maranga** – Asante Said Muhammed. Tafadhali tuwekee sahihi kitabu chetu rasmi na nashukuru kwa maoni yako. Mwingine anaitwa Toash Maro. Toash Maro?

**Toash Maro Ayub** - Majina yangu ni Toash Maro Ayub. Jambo langu la kwanza ni kwamba wakati mwingine uwa mutu amashikiwa, kama pengine ameiba. Lakini hakuna uhakika. Sasa kwa sababu ya kushikiwa, mutu huyo anateswa, anapigwa, mwisho anakubali kwa jambo ambalo hakulitenda kwa sababu ya kuhepukana na kile kipigo. Kwa sababu hiyo ninge onolea kwamba, kama jambo hilo liko katika Katiba ya mbele, libadilishwe, ili kuliko kupigwa na kuteswa, kuwe na njia nyingine ya kuhoji huyo mutu, hatakubali.

Na jambo la pili, wakati serikali wanapo fikiria kuongeza mishahara ya wafanyikazi, wa Bunge na wafanyikazi wa serikali, hapo mwananchi yule ya kawaida, hakupangiwa chochote. Kwa hivyo ninge penda kwa Katiba hii ya sasa, badala ya kumwongezea pengine mishahara wafanyi kazi wa serikali, na wabunge, pia mwananchi yule wa kawaida naye afikiriwe kitu kidogo chakumuendeleza katika maisha yake. Nafikiri kufikia hapo, yangu ni hayo. Asante.

**Com. Maranga** – Asante Mzee. Toash Maro. Sasa utuwekee sahihi kitabu chetu rasmi. Anayefuata anatiwa Joseph Mbawu. Joseph Mbawo

**Joseph Mbawo Rukaria -** Kwa majina naitwa Joseph Mbawo Rukaria Mimi ni mkaaji wa Kipini Division. Kwanza mimi nataka kusungumuzia habari ya elimu. Wakati mimi nilianza kuerevuka mimi nilivalishwa uniform nikapelekwa shule. Lakini sikuona mzazi wangu akilipa hata ndururu. Kwa hivyo tunaomba Team wa urekebishaji wa Katiba upande wa elimu iangalie

sana, kwa sababu masikini wame kuwa ni wengi, hawawezi kusomesha watoto, kwa sababu fedha zimekosa value.

Upande wa afya. Nikikumbuka mimi vizuri 1977 huko, nilikua naenda hospitali, mimi na ugonjwa wangu pekee yake, kwa sababu serikali ilikua inaangalia habari ya afya kwa bure. Hakuna kitu mutu alikua anaitishwa hata Kadi. Kwa hivyo tunomba team wa urekebishaji wa Katiba iangalia hiyo haki ya binadamu, kwa sababu binadamu ni kitu muhimu kuliko mali.

Upande wa ufisadi. Sisi tunasema team ile imechaguliwa ichunguze wale wametufanyia serikali ufisadi. Hawo watu wakishaa patikana, wananchi wote wajulishwe na ile mali yote wameibiya wananchi irudishiwe wananchi ili waweze kujiendeleza, ili tuweze kukaa sawa.

Upande wa ukulima. Unakuta mukulima analima mali yake ajisaidie, lakini badala ya ajisaidie, uwa inasadia broker. Kwa hivyo tunaomba serikali katika team wa urekebishaji wa Katiba, irekebishe, serikali isimamilie mukulima, ili mukulima aweze kunufakia na mavuno yake. Asante ni. Ni hayo tu.

**Com. Maranga –** Asante. Weka sahihi na nashukuru kwa maoni yako. Mwingine ambawo tunataka atoe maoni yake anaitwa Bwana Omar Babu. Omar Babu? Omar? Karibu.

**Mzee. Omar Babu -** Naitwa Omar Babu. Nasikitika sana manaake maoni mengi yame tolea na kule kurudia naona hakuna haja sana, isipokuwa nina maoni ya kuongeza kidogo. Kwanza mimi ni Muislamu, kwa hivyo kama kawaida ningeomba kuwe na uhuru ya kuabudu kama ilivyo hivi sasa.

Cha pili, kuna sheria katika Uislamu jinazo husu ndoa na uridhi na zile sheria vile vile jiendelee kwa sisi Waislamu.

Tatu. Nikiwa katika hiyo sehemu, katika sheria za KiIslamu ambazo zina hukumiwa na ma Kardhi, kuwe na ma Kardhi katika viwango tafauti. Kuwe na Kardhi wa Wilaya, alafu kuwe na Kardhi wa Mkowa ambaye itakuwa ni High Court, na kuwe na Court of Appeal. Ili kutowa nafasi kwa wenye kujiteteya, wajitetee haki zao ziweze kutekelezwa iwavyo.

Nikitoka katika hiyo sehemu, ninaenda katika Provincial Administration. Mimi kwa upande wangu, naona mwenendo wa sasa kwa Provincial Adimistration, tugewuze ili watu kama DC, watu kama PC wachaguliwe na wananchi badala kuwa watu wa serikali kwa sababu ndiyo watu wakichaguliwa wataijibika zaidi. Kwa sasa corruption inaendelea kwa vile mutu anatoka mbali, anakuja sehemu ambaye si yake, na katika usumamizi wa miradi na pesa za serikali hawezi akajali. Anaweza kufuja hizo pesa, na ile miradi.

Chengine ningependa aah…. mutani samehe kidogo kwa sababu nilikua na homa wiki mbili, na hata kwandika karatasi sikuweza, ndiyo unaona kidogo nimefanya kusao yale ambawo nilitaka kusungumuza.

**Com. Maranga –** Asante. Kwa hivyo unataka kukomea hapo?

**Mzee Omar Babu –** Siku maliza. Kuna jambo muhimu zaidi.

**Com. Maranga –** Lakini unaweza kutuandikia. Alafu ututumie Nakala zako Nairobi.

**Mzee Omar Babu –** O.K.

**Com. Maranga –** Kupitia kwa either District Co-ordinator ama moja kwa moja.

**Mzee Omar Babu** - Hivi sasa.Asante.

**Com. Maranga –** Asante. Nashukuru Mzee Omar Babu. Mwingine ambawo tunamtaka aongee ni Omar Galana.

**Omar Galana –** Mimi jina yangu ni Omar Galana Hirbai. Na sijaelewa ninataka, nimepatiwa dakita tano, nimeomba mbili ziwe saba. Na maoni yangu, ni hajatajwa nafikiria. Maoni yangu ni majimbo. Nasababu kutaka majimbo kwa Katiba sababu kukosa majimbo imekua Kenya imekosa heshima. Watu wageni wanaingia Kenya, wanavuruga amani yetu na tumefungua macho tukakutwa wakati wa wingereza kulikuwa na majimbo, na wakati huwo wa mwingereza, mutu akitoka North Eastern, kuingia Tana River, anakuja na pass. Sasa sisi maoni yetu leo ni majimbo. Sijiu watu hawaja taja, sijui wana nini wala nini, lakini kama mimi maoni yangu ni majimbo.

Kitu ya tatu. Hata ujambazi unazidi kwa sababu ya majimbo. Mutu anatajirika kwao. Anachukua mbunduki kwao, anakuja Tana River, anakuja kuvunja duka, kuchukuwa ngombe, mutu afanyi biashara pali popote, kwa sababu yeye ametajirika huko hataki wengine watajirike. Kwa hivyo kama mimi maoni yangu ni makubwa ni majimbo.

Kitu cha nne. Ardhi. Ardhi tunayonyanganywa ni wenye pesa na si watu wa Mkoa huu wa Tana River. Tukikaa mbeleni watoto wetu na wajukuu wetu watakosa ardhi, kwa sababu ya wageni, mutu atatoka North, mutu atatoka Nairobi ata kuja hapa bila ya kuona wenyewe. Anapata ardhi kwa jili ya pesa. Na jee, watoto na wajukuu wetu tutawaweka wapi? Kwa hivi maoni yetu, watu wengine ni majimbo, sababu mutakua na heshima, ataingia kwetu, Tana River na kuomba, nakujulikana huyu ni nani huyu ni nani. Kwa hivi sina mengi zaidi, nina omba sisi Tana River hasa, ardhi iwe ya wenyewe na tupate uchumi kama mwingereza, maanake mwingereza ni mwingereza ametupatie uhuru lakini kukawa na nini, na majimbo. Mutu wa Nairobi hakuingia Tana River. Mutu wa Tana River hakuingia Nairobi, mutu wa North hakuingia Tana River, mutu wa Tana River hakuingia huko bure bila baruwa. Kwa hivi maoni yangu ndiyo hayo.

**Com. Maranga** – Asante Mzee Omar Galana. Nakuomba tu utuwekee sahihi na asante kwa maoni yako. Weka sahihi kitabu chetu rasmi. Mwingine ambaye anataka kuongea ni Ali Titila. Ali Titila?

**Ali Titila** - Ndungu Commission na wananchi wezangu, jina langu ni Ali Titila. Ile Commission ambayo ilikua imekaa mwanzo. Commission au Covenant ambaye ilikua imeandika Katiba ya mwanzo, ilikua na mawazo sana ya kimagaribi. Ilisahawo mila na desturi za mwafrika hasa ukifikiria upande wa kina mama na watoto. Hawa watoto na akina mama upata mateso sana. Hasa ukifikiria wakati mzazi au mtoto wa moja katika hawo amefariki. Kwa mfano ukitembea bara barani, utaona jeneza zinapita au Coffin, ukiuliza, ni nini ile, wanakujibu kirahisi, ni mtu, lakini wanasahao ya kwamba yule anaenda kuzikwa ni mpenzi wa mutu fulani, ni bread winner wa mutu fulani, au ni mtoto wa mutu fulani, au ni mzazi wa mutu fulani. Mateso yanapo kuja, ni yule mutu baada ya kuzikwa. Katika hakimiliki za mtoto na mama. Hasa kwa upande wa Waislamu. Ndiyo utaona kuna mateso makubwa. Ukitazama, pengine kutakuwa yule baba aliefariki ni mfanya kazi ya serikali na mama pia ni mfanyi kazi wa serikali. Katika desturi za Kiislamu, mama anapofiliwa, anatakiwa kukaa kwa eda kwa miezi mi nne na siku kumi. Hiyo kama yeye ni Mdaktari au ni Mwalimu itambidi aende akakae kwenye nyumba bila mapenzi yake. Na serikali au Katiba yetu haina coverage ya mutu kama huyu ya kwamba kwa vile amekaa ndani, na si mgonjwa ni sheria tu imemuweka ya Kisislamu, yakwamba atalipwa mshahara wake. Anaambiwa wewe unatakiwa uende uchukuwe unpaid leave, ambawo sasa akichukuwa unpaid leave, yule mama ambayo yuko ndani ya nyumba, atakula nini, atasaidia nini watoto wake? Kitu kama hichi kinatakiwa kiangaliwe. Tena utakuta pengine mtoto wa mzazi kama yule ambaye amefariki, yeye ni under age, pengine baba yake amemufungulia account kwa bank fulani, na mtoto yule ile pesa ataambiwa hawezi kuipata mpaka afikie at the age of 18. Je, wakati huwo akiwa mdogo, mtoto yule atasoma na nini? Na baadaye basi kama hizi zina chukuwa hizo pesa na kupeleka kwa Public Trustee. Wakipelekwa Public Trustee mtoto anapo kufikia at the age of 18, kupata hio pesa inakua ni kazi kubwa ya ajabu, ambayo hata saa ingine wanaenda wana dispare. Kwa hivyo sheria kama hizi, zinatakiwa kidogo wazichunguze na wazitazame vizuri. Asanteni.

**Com. Maranga** – Asante Ali Titila na nakushukuru kwa maoni yako. Tafadhalini uweke sahihi kitabu chetu rasmi. Mwingine ambaye ninamwita sasa kutowa maoni yake ni Shariff Abdulkadir. Shariff?

**Shariff Abdulkadir** - Asante. Jina langu ni Shariff Abdulkadir, mfanyi biashara. Maoni yangu ya kwanza ningependa serikali kuhusu mambo kwa Katiba huu uwezo kwa upande wa DO, Chief, Sub-Chief unge sukumwa kwa wazee. Tuwe na baraza la wazee ambapo tutawafanyia uchaguzi kila baada ya miaka miwili na baraza la wazee hawa, yale marupu rupu unaopitia kwa ma DO, kwa ma Chief iwe na wawo watangalia. Ili wawe na morale ya kusimamia mambo kama hayo.

Jambo la pili. Naona wezangu wame ongea kwa upande wa afya, mambo wa hospitali. Lakini kuna jambo muhimu sana naona hawakuelekea manani. Hapo hospitali yetu, wakati sisi tunafahamu, hospitali hii ilikua ina pesa kutokea wakati serikali ya mkoloni. Hospitali hii ilikuwa na pesa yake ikitumania ikinunua madawa kwa pesa zake, ya baadhi ya mambo tofauti tofauti. Na leo tunaona pesa hizi ni kama zimekatua haziji, ndiyo imekua sasa watu wanalipishwa pesa na wengine hata hawajimudu,

kwa hivyo tungeomba kipengele hiki kwenye Katiba hii hospitali yetu ijaribu iangaliwe pesa zile zirudi. Ili hospitali yetu ipate huduma kama hizi.

Na maoni mengine. Tunashida sisi ya barabara hii, baiyana hapa na Garsen, ama tuseme Gamba, na serikali tiyari twasikia kuna pesa ambawo zimetoka kwa barabara hii kuanzia Garsen mpaka Lamu kufanya ukarabati. Kwa hivyo tungeomba na sisi, wana Kipini ambawo barabara yetu kutoka Witu na hapa, ni kilometer ishirini na mbili, wakati urakabishari wa barabara ile wa kwenda Lamu, na sisi tupate lami kutoka Witu mpaka kuingia Kipini, iwe ndani ya mapendekezo ya mwamukua wa hii Katiba mpya.

Lingine nikuhusu habari ya wanyama. Hapa tuna wanyama wapori ambawo mwananchi mwanya ule anaweza kumsaidisha. Tunaona serikali inatoa leseni kwa watu binafsi au watu maalumu ya kupiga wanayama hawo. Kwa hivyo tungeomba na sisi wananchi mwamuko huu wa Katiba mpya wanyama hawo na sisi tupewe vibali hizo, na sisi tuweze ku shine na wanyama hawo, sababu tunawengi wetu hapa watamani kula nyama ya Kiboko, Tope, Nyati na wanyama hawo tuko nawo hapa, hata serikali kama itatupatia vibali wa kukunua mapato mengine iingie kwa serikali na mwananchi naye ajivunie na wanyama hawo.

Jingine langu la mwisho tutarudia upande wa ardhi. Nafikirri upande wa ardhi imezungumuziwa kirefu sana. Lakini hatujaona mwamkwo. Siala la mambo ya ardhi tunataka irudie kwa Kamati za wazee. Si mutu uko Nairobi, anapimiwa ardhi, anyanyakua kwa njia ya juu. Nikama hapa kuna sehemu inaitwa Prison Farm. Prison Farm hii kumetoka vibali. Watu wengine wa Nairobi, wa hapa na tiyari kuna ma squartter ndani zaidi ya miaka ishirini. Na leo mwanamushule ule ule ukipitia sehemu ma Tangeni mpaka kufika Kuzuiliani hizo sehemu zime sha nyakuliwa, watu wame kaa ni squartter na hawana kitu. Kwa hivyo tungeomba serikali kulingana na mwamkwo mpya wa Katiba hii, jiwe cancel hizo zirudishwe kwa wazee, zigawanyiwe wale ambawo wana haki ma squartter mapate haki zawo. Yangu nikifupishia nafikiri ni hiyo tu. Ime tosha.

**Com. Maranga** – Asante bwana Abdulkadir. Tuweke sahihi kitabu chetu rasmi na asante kwa maoni yako. Mwingine anaitwa Musa Guiyo. Musa Guiyo?

**Musa Guiyo** – Kwa jina naitwa Musa Guiyo. Yangu ni mawili ambayo kwamba isha sungumuzwa lakini kwanza ninge changia ilo swala la wanyama. Ukweli ni kwamba, kutoka historia, hata huyo Mungu aliumba mwanaadamu alimuweka juu na wanyama walikuwa chini. Lakini inaonekana sasa mnyama ana thamani kuliko mwanaadamu. Masahamba wa wananinchi wanaliwa na wanyama na ukiwapelekea shida hiyo wale wame husika, ata unaulizwa, je wali umiza mwanaadamu ama ni wanyama, hata uwezi kupata zibu. Kwa hiyo wananchi ambawo kwamba ni wakulima wananyanyaswa sana kwa sababu wanyama wanakula mimeya na hakuna fidia kwao wakifa au kwa sehemu zingine lakini. Sehemu zingine za Kenya hakuna fidia ya mimea, wala pengine wawe wakiumizwa. Kwa hio ningeomba katika Katiba hii ambayo kwamba inarekebishwa, mwanaadamu apewe haki yake kwamba yeye ana thamani kuliko mnyama.

Jambo la pili, ni kuhusu ardhi. Mimi ningechangia Katiba ya Kenya, kwa mambo ya ardhi. Najuwa kwamba Kenya ina sehemu nyingi na inamakabila mengi, ina watu wengi. Na bahati Mwenyezi Mungu, kila watu waliwekwa sehemu tofauti na wengine, hata kwa lugha. Kwa hiyo mimi ningechangia kwamba, wazee wa sehemu yoyote ya inchi, wanapo gawanya sehemu yao kwa watu tofauti, tofauti, ili kupewa stakabadhi au Title Deed, wagawanyiwe na sehemu zile ambazo kwamba zina bakia, sehemu kubwa, ziachwe chini ya mamlaka ya wazee, wa sehemu ile. Kwa sababu ya vizazi vinavyo fuata. Yangu ni hayo mawili. Asanteni sana.

**Com. Maranga –** Asante mze Guiyo. Musa Guiyo. Sasa tafadhalini tuwekee sahihi katika kitabu chetu rasmi. Mwingine anaefuata ni Bakari Ali Hirbai. Bakari Ali Hirbai?

**Bakari Ali Hirbai –** Kwanza kwa majina yangu mimi ninaitwa Bakari Ali Hirbai. Kwa hivo, muchango wangu kulingamana na Katiba, kitu cha kwanza ni kupitia upande wa Urais. Upande wa Uraisi, kama vile ambapo tulikuwa tukitawalia, tunataka kama ikiwezekana, Raisi apate kura asili mia hamsini. Akishindwa kupata asili mia hamsini, huyo haja kuwa rais. Moja.

Mbili. Tunataka kitu umasikini. Bado umasikini hapa haujatajwa. Lakini, mimi nitataja kwa sababu sisi ni masikini. Kwa hivyo kupitiya umasikini serekali tunataka iwasaidie wananchi kupitiya kwa matingatinga kwa saidia kilimo cha mashambani, kipindi cha miaka mitano. Wakimaliza miaka mitano, wataangalia vile hali ambawo wananchi wanaipata. Mbili.

Tatu. Tutaongea kuhusu upande wa majimbo. Niyatatu lakini kwa upande wangu mimi, naona ni ya kwanza. Majimbo ndiyo haki zetu. Kwa sababu majimbo yatakua karibu na wananchi. Yale mahitaji ya wananchi ambako ambawo wangeyataka kutoka kwa serikali, ni kupitia kwa njia ya majimbo. Kwa sababu rais atakua yuko hapo, serikali kuu yuko hapo, kwa kila kitu atakipata huduma ziko hapo, kwa hivyo mimi naonelea kwamba katika haya matatu, majimbo iwe ni kitu cha kwanza. Kwa hivyo hayo matatu, nasema asanteni.

**Com. Maranga –** Asante Bw. Bakari Ali na nakuomba uweke sahihi kwenyi kitabu chetu rasmi. Mwingine ambayo ninamuita ni David Nyamu. David Nyamu?

**David Nyamu –** Kwa jina langu naitwa David Nyamu. Mimi nimukulima, kutoka Tundu. Mimi nasungumuzia mazingira ya mwananchi sababu ni kwamba, nasungumizia habari ya wanyama wa pori, hata ikiwa imesungumuziwa. Hiyo ndiyo ilikuwa maoni yangu. Kwa kuwa wanyama wa pori na mwanadamu ni tofauti. Na wanyama hata Mungu nikweli aliumba wanyama na akaumba wanaadamu, akawambia Adamu mwenyewe awape majina. Na wakati aliwapa majina, walikuwa chini yake. Hata tuna angalia mpaka upande wa Nugu, alipewa tena wawe chini kabisa. Leo hii wanyama wanasumbua watu mashambani. Na ukienda huko, kama mimi Nyamu, safari ya kwanza nili liwa na Nyati, acre tatu ikaisha. Asubuhi yake nikiamuka nikakuta hakuna indi hata moja. Kuja hapa niliambiwa niende nikaweke fence, na hakuna malipo. Niliumia mwaka huwo wote na njaa. Nasikupata chochote.

Mwaka huo ulipita, huu mwingine ulipita huyu nili liwa na Kiboko tisa, walikuwa tisa kwangu shambani. Walikula mahindi yangu yote, na waka funja funja pamba yote. Na niki endelea kusema, nikambiwa niende nikaweke fence. Hakuna malipo. Sasa ninaauliza swali langu, ile ningeuliza Katiba iendelee, serikali iweke katika Katiba, ni kwamba, ikipitisha, ipitishe hio, mwanaadamu awe aki ifadhiwa kwa malipo, akiwa ni maindi, kama nini kimekulia au imeharibiwa na wanayama, awe ni wakwanza kulipiwa aka angaliwa sana, sababu anaumia kule mashambani hakuna musaidizi. Sababu ya kusema hivo ni kwamba, mimi naona watu wengi, watu wengi wako musituni, kwa mashambani, wana adhirika sana na hiyo mambo ya malizo ya wanyama. Na sioni hata wakiangaliwa. Kwa hivyo mimi ningependelea ya kwamba wawe wakiangaliwa wakati wote, wakati wakilimo ndiyo wawe wakiangaliwa.

Tena turidi upande wa utawala. Upande wa utawala, ni kwamba hapa hatuna uduma wowote kabisa katika watu wa mashambani. Huduma yetu aipatikani kabisa katika serikalini, kwa maana hapa serikali yote sijui hata serikali ya hapa kwetu sijui ni namnagani ni kwamba haiangaliwi kabisa. Wale waliandikwa kama ma Chifu na DO, hapewi hata gari, gari ilipeyanwa hapa ni hasara, hata isaidii chochote hapa. Sipitali haina gari, mgonjwa akipatikana hapa kama muja muzito apati gari kabisa, kabisa niku umia hapa.

Ukiangalia upande wa polisi nawo, polisi hawana gari kabisa, kabisa ya kwenda kuhudumia wananchi katika mashambani. Mashambani yetu, yani tunaumia kwa kila jambo, ndiyo ningependelea ya kwamba, ikiwa ni hapa, DO apate gari nzuri, ya kuwa inasaidia mashambani, ikiwa ni polisi, wapate gari ya kusaidia, ikiwa ni pale hospitali, nawo ipate gari ambaye ya hudumia mgonjwa. Tupate kufaidika. Kwa maana hata tukiwa tukiumia pale, maanake pale ni kutasa, tukiumia tukipewe huduma, tukuiandikiwa Lamu ama Mombasa, ama huko Hola, hakuna gari ya kwenda huko, mutu ukufia hapa. Mimi nakumbuka siku moja, bibi yangu alikua mgonjwa, alikuwa mgonjwa kabisa, mimi niliomba Mungu kwa kitanda pale nikapiga magoti hata ule daktari alikweko, ule Mumeru akaaja kulia, kwa maana yule bibi tuliona nakufa, na hakuna huduma wowote, Mungu aliniletea gari kuto huko (Lorry) ndiyo ilibeba bibi yangu mpaka Lamu, na nikashukuru sana.

Kwa hivyo ningependelea ya kwamba Katiba ikipitishwa sehemu kama hizi ndogo, Location kama hizi ndogo, zika angaliwa sana, ndipo wananchi wakapata kusaidika. Sababu sisi ndiyo tunaumia. Hata tukifanya nini, hatuna uwezo wowote ajapo kuwa sasa tumletewa uwezo ama mambo ya kusaidia karibu, tuje tuseme hapa maanake hakuna officini tutaenda. Tukitamani kwenda officini pesa hakuna, hakuna mpango wowote tunaenda kufanya. Ukiambia mutu tuunganishe pesa tuende officini tukatete, hakuna mutu yaku kubali. Maanake pesa hana. Sisi tumebaki masikini. Ndiyo tunasema leo tuna bahati nzuri ya kusema ya kwamba tume bahatika kuja kusema maswali yetu hapa. Naomba kwa serikali, Katiba ipitishe mswada huyu wa wanyama wa pori, na muswada huyu wa kuangalia kama Location yenyewe inakaa ndiyo, DO wa tarafa apewe gari mzuri. Na ndipo basi apate kuhudimia wananchi. Asante.

**Com. Maranga –** Asante Bw. Nyamu na utuweke sahihi kwa kitabu yetu rasmi. Mwingine ambayo mimi namwita ni Keya Bagaja. Keya Bagaja? Ako? Keya? Ndiyo hiyo? Bagaja?

**Keya Bagaja –** Mambo matatu lakini yame tajwa. Lakini nitaguzia mambo mawili ama matatu. Ardhi, Mali ya asili, na Economy. Wale wanaotoa ardhi kutoka Nairobi tabiya hiyo waiache. Maanake hapa wanaokaa ndiyo mali yao. Inapasa, mwenye kutoa ardhi, ikiwa anatoa ardhi, aje aone, anaye kaa ardhi ile yuko wapi. Si kutoa kule waje wamondee anaye kaa kihalali amezaliwa pale. It is very unfair. Hiyo ni moja. Na njia ya kutowa hiyo ardhi, iwe kunahusishwa watu wa County Council, una husishwa, Provincial Adminstration pamoja na wenyeji pale. Isiwe mutu anakwenda Nairobi, ana andika anakuja kuchukuwa tu ardhi namna hii.

Na jambo la pili, Mazingara, mali ya asili. Tunawo manyama kama vile tunawo watu. Lakini watu, wanatawala wanyama. Tayari tumeona wanyama wananyanyasa watu, na mutu ana mteteya munyama, na munyama anakuwa na dhamani zaidi ya mutu. Kwa hivyo tuwashauri katika Katiba kwamba hawa wanyama wawe wanalindwa na wananchi pamoja na serikali, lakini wa hakikishiwe ya kwamba wanyama wana heshimu watu. Wasije wakala, wasije wakaharibu, wasije wakadhuru… Wawekwe kwenye miji yawo. Na ikiwa wanakuja kuharibu mali ya watu, waondolewe ama wawawe, maanake hawana dhamani kwa watu, na ikiwa wanawekwa kwa ajili ya utalii, si wapelekwe kwenye Game Parks, wawekwe huko watu watawaona. Lakini Yonda na Tumbiri aje ale mali yako na huna chakula nahuyu anaokatia hidi yuko Nairobi, yeye anapiga shilingi mwisho wa mwezi ale, wewe unakwenda njaa umikwisha sikia, Game Park na mnyama. Na wale wanaokufa kwa ajili ya wanyama walipwe mara moja sio kwenda kurudi, kurudi, kwenda mpaka mutu akose tumaini na aache habari yake.

Habari ya mwisho ni economy ya Kenya kama vile tunavyo sikia ime enda chini kwa vile garama za maisha zime kuwa juu. Na misada hii katika Katiba tukiomba tuiweke ifikie wananchi hasa wale wenye uhitaji. Tumesikia tayari uhitaji wa barabara. Labda wakati wa El Nino kulipata msada. Gamba mpaka leo inaviki. Hola, Garsen inaviki. Na kama tumesikia vizuri pesa zime toka. Ili pesa hii ya msada imeotoka iwafikie wananchi wale wenye uhitaji na tena tuhakikishe ya kwamba pesa hii iki ingia ilipie maisha yawe raisi kidogo. Yatakua raisi namna gani? Kwa mfano kwa wakulima wapate misada ya mbegu, wapate misada ya tinga, wapate misada ya visima vya maji, ili watu wanaosumbuka kuranda randa na wanyama kwaajili ya kulisha, watakua na visima vyawo, watakua na maji yawo, hawata sumbuka kuranda randa. Lakini kwa vile maisha ni magumu, wanalazimika kupigania haka ka chochoro ka mtotana, na hata wale wenye mashamba wananga'nga'nia huwo karibu na mto kwaajile ya maji, lakini wakipata visima, wakipata mfano kamili wa mashamba ya Tinga basi hata maisha chakula anapata, wanyama hawa wadhuru. Bengu na dawa zinapatikana kwa kupitia misaada hiyo ya kupunguza garama. Labda wenye shida watakuwa ni watu wa town. Na town pia watapata misaada hiyo kwa kuona garama ya vya kula na vitu vingine vime lipiwa na kupunguzwa na misaada hiyo madukani na relief itakuwa kamili. Asante sana.

**Com. Maranga –** Asante sana na utuweke sahihi kidole kitabu chetu rasmi. Mwingine ambaye ninayemuita ni Ester Dulu. Ester Dulu?

**Ester Dulu –** Hamjamboni wananchi? Mimi kwa jina naitwa Ester Dulu na ni Chairlady wa Maendeleo Ya Wanawake katika

Tarafa hii. Kwa hivyo nikianza kusungumuzia ni kwamba, (interjection by Com. Maranga)

**Com. Maranga** – Mama kama una memorandum unge toa tu ile maoni muhimu. Hiyo memorandum utatupatia sisi. Utupatie ile points muhimu kwa sababu watu ni wengi wanataka kuongea na muda ndiyo huwo ina yoyoma.

**Ester Dulu** – Sawa. Kwa hivyo nikiweza kuongea kwa ufupi ni kwamba, Kenya ilikua haina utangulizi katika Katiba hii iliokua tukiendelea nayo. Na nafikiri tulipata kujua kwamba ilikua ni Nchi yetu ya Kenya haita tawaliwa na mutu yeyote, hata siku hiyo tukaweze kumu uliza maswali alie tuelimisha, kwa hiyo nikusema kwamba hata huyu President tulio naye, naye pia bado sie mutawala wa nchi yetu. Kwa hivyo hapa nina utangulizi kidogo kwamba Wimbo wa Taifa kama ulivo unavyoendelea, uendelee hivyo hivyo. Na utangulizi wangu ni hivi Katiba ya Kenya, ilio jadiliwa na kukubaliwa na wa Kenya wote kwamba, tutalinda mali asili ya nchi yetu ndani na hata inje ya Kenya.

Nikiguzia kidogo kwa habari ya wabunge, wabunge wote wameajiriwa na wananchi. Maana kabla hatuja wachagua, hawataitwa wabunnge, nawale hawataenda kule Bunge. Lakini kitu ni kwamba walipo enda Bunge, wanapindwa pindwa mambo, vile wanavyo penda wawo. Wanamsahawo yule aliempeleka kwamba ndiye tajiri wake, kukiwa na jambo ni awamuulize maoni ndiyo wafanye kazi zao. Kwa hivyo kwasababu hiyo waka badilisha badilisha sheria kadha wa kadha katika miaka thelathini na sita wakabadilisha mara thelathini na saba. Kwa hivyo wakati huu kulipo fumbuliwa habari ya Katiba kurudi kwa wananchi, tumesema asante, na iwe hivyo.

Tukienda habari ya mishahara, wabunge wanajititea wawo zaidi. Mutu anapata elefu mia tano mbali na yale marupurupu ya kwenda hapa na pale. Kama msemaji alivyo sema Headman ambaye kwamba kukitokea hali ya serikali hapa anafuatwa hata akiwa musituni, anazunguka jua hili lote, lakini hana ndururu anaolipwa, naye mubunge analipwa elufu mia tano. Hebu haki iko wapi? Kwa hivyo ni vizuri kwamba wale ni viongozi kweli, lakini wakijua kuwakumbuka wale wanyonge, walio nyuma, maana bila wale wanyonge hata hawo hawafanyi kazi.

Na pia tunambiwa kwamba serikali ya Kenya uchumi umezorota. Wakati tumepata uhuru, sitini na tatu, nikusema kwamba kila kilicho Kenya hii ni chetu. Lakini kuna ma Title Deed yanayo sema miaka miya iliopita. Nahali uhuru tumeupata, lakini zile Title Deed zilizoandikwa wakati wa mukoloni, hazija katwa mpaka saa hii. Maana kama ni Title Deed za halali, zingeanzia mwaka wa sitini tatu mpaka leo, ndiyo uhuru kamili. Lakini unasikia sehemu hili ni la mzungu, Mutaliano, sehemu hili ni ya Mwarabu yuko Zanzibar, kwa hivyo tumekaa hizo sehemu zilizo andikishwa hivyo ni kama masquartter tu sisi tuna kaa. Sasa uhuru kamili, mini kivyangu sijauona, kwa sababu hizo kadha wa kadha zilizo chukuliwa wakatu wa ukoloni na tulipo pata uhuru pia, hayakuchukuliwa maanani.

Kisha basi tulipo pata uhuru, baada ya serikali kujua kwamba wale wakaaji waneoilo wapate ma Title Deed, hawakufanya hivyo. Wamemutoa mzungu, kisha wazungu akawa ni wawo, maana wawo ndiyo ma officer, ndiyo viongozi, waka andika

andika hizo sehemu wakachukuwa wawo tena. Kumsahawo mwananchi kwamba naye anaishi hapa, kwa sababu mwanainchi haku soma hajui chochote, kwa hivyo ikawa ni rahisi kuzichukuwa hizo sehemu aziandikiwe wawo wenyewe, na mwananchi abaki pale masikini milele na milele. Kwa hivyo inaonekana kwamba viongozi wanajitakiya wawo zaidi kuliko kumfikiriya yule mwananchi ambaye wamekuja wakamkuta pale, ingaweje ajui customary lakini naye ana haki zake kwa sababu anaishi pale.

Na habari ya elimu, I mean ufisadi. Tunaambiwa ufisadi unaendelea. Kwa nini uendelee? Wako viongozi. Kukiwa kuna haribika jambo, kwa nini wale viongozi hawawezi kulichungulia na wali simamishe mara moja? Tunajua kwamba katika dunia saa hii Kenya inasifa mbaya ya ufisadi. Wanasema uchumi imezoroteka, hizi pesa wanaziunda vyama vingi, wakaaja huku, yule ni chama, yule ni chama, wanazitoa wapi? Na wanasema Kenya imezoroteka. Hizi pesa zina toka wapi? Kwa hivyo kama vyama vinge kua viwili ama vitatu, tunge kuwa na garama ndogo zaidi na hali zetu za Kenya ziwe zinaendelea.

Pamoja na hivyo, wako viongozi wa Kenya wanachukua pesa za Kenya, na kuweka bank inje ya Kenya, ambazo kwamba kule zinakoenda, zinafanya biashara Ulaya, zinafanya biashara wapi, faida zote zina kaa kule. Sasa kama hazikuwekwa humu Kenya, zifanye bisahara za Kenya, zizalishe mambo za Kenya, uchumi utaendeleaje mbele? Na pesa zinatolea Kenya zikitoka inje. Kwa hivyo viongozi ndiyo wanamaliza hii Kenya. Pesa natowa inje, vibali wanajiandikiwa wawo, mwananchi saa yote yeye ni shida kwa shida.

Na wakati mwingine mavuno, ama biashara za kuhusu mukulima. Ukisikia biashara yoyote umewekwa beyi ya juu. Tunajua kwamba hiyo biashara imehusika na wale viongozi ndiyo lengo wanalolilima wawo. Kwa hivyo biashara ..(interjection by Com Maranga).

**Com. Maranga –** Hiyo ni onyo mama.

**Ester Dulu –** Sawa.

**Com. Maranga** - Saa ime yoyoma.

**Ester Dulu –** Haya. Kwa hivyo biashara fulani imepanda, ni sababu viongozi fulani wanalima mumeya ule. Kwa hivyo ndiyo unaopiganiya kule Bunge mpaka iwe na hali ya juu ili wapate wawo vingi. Lakini huu mukulima wa chini ni shilingi mbili, ni shilingi tatu ndiyo biashara ya mukulima wa chini. Kwa hivyo pia serikali alianglie jambo hili. Kwa sababu wanavyo lima wawo, ndivo tunavyolima sisi. Sikua waangalia mavuno yawo na mavuno ya mukulima ya aachwe.

Na hali ya barabara kama munavyo sikia ni mbaya hata saa hii maembe yote yame zaa sana. Mbwa zita anguka saa hii. Hatuna pa kuzipeleka. Na unasikia kwa maradio million tatu zime toka, million kumi zime toka, na huoni chochote kilicho iendele. Kwa hivyo pesa zina toka zakutosha ziko za waKenya lakini zinamezwa na viongozi na sisi wananchi tukiumia huku,

bidha zinaoza, mambo mengine hatujulishwi, wala hatu andikishwi , kwa hivyo muanangalie.  Zangu ni hiyo.

**Com. Maranga –** Asante mama Dulu kwa hiyo maoni na ujiandikishe na utupatie hiyo memorandum yako.

Mama Ester Dulo – Sawa.

**Com. Maranga -** Mwingine ninayemuita, nataka uwe kwa ufupi kabisa tafadhalini, mutoe maoni kwa ufupi kabisa, Omar Ngama.  Omar Ngama?

**Omar Ngama –** Kwa jina naitwa Omar Ngama.  Maoni yangu ni ya fuatavyo.  Kuajiriwa kwa kazi katika Wilaya, wachukuwe kila Locationi.  Kwa sababu inafanya raia katika sehemu wawe na utamu wa kusoma na kujisikia huru.

Mbili: wafugaji wawe mbali na wakulima.  Hii ni kutofautisha kuleta muzozo kati ya wafugaji na wakulima.  Hasa wale walio kando kando ya mto.

Raia anapo fanya makosa, basi wale polisi wamuchukuwe waende naye asimalize ma saa kumi na miwili kufikishwa mahakama.

Na ardhi ambawo imichukuliwa kwasina ivi niya wenyewe irudishiwe wenyewe kisha yule mutu ambaye amechukuwa ile ardhi awafuate kamati hiyo katika Location hiyo.

Lingine ni kuwa sisi tu Waislamu, na kuna namna mutu anewaze vaa.  Wasichana siku hizi ndiyo wanaleta shida za kunajisiwa kwa sababu wa huo nguo wanavo vaa.  Transparent clothes, nguo ambazo hivi zinazo onyesha wazi wazi.  Wasichana kama wawo wachukuliwe hatua, kwa sababu watapunguza shida hizi za kunajisiwa na magonjwa wa ukimwi.

Lingine ni kuwa kwajiriwa kwa kazi iongezewe miaka ikiwa intawezekana katika sheria hizi kama vile askari, miaka kumi na minane hadi kidogo thelathini.  Maoni yangu ni hayo.

**Com. Maranga –** Asante Omar Ngama.  Utuwekee sahihi kitabu chetu rasmi.  Mwingine ni Mohamed Said Dawa.  Haya haraka haraka.  Watu ni wengi.  Watu ni wengi wanao taka kutoa maoni.  Kwa hivyo fanya haraka haraka.  Muhamed Said Dawa.

**Mohamed Said Dawa**  - Kwa majina, naitwa Mohamed Said Dawa, Headman Kipini Town.  Kabla sija enda kwa mchango wangu, kwanza natoa shukrani kubwa sana kwa nafasi hii, ambayo niliopata kuchangia Katiba hii mpya.  Kwa sababu nimechukuwa kwa mfano vile nime elewa, nimechukulia kwa mfano nikama ule mtoto mchanga aliozaliwa leo, ambawo amemutegemea mamake ndiyo ile Katiba ya leo ambayo nataka kuichangia.

Nikitaja yale ambawo nitachangia. Kulingana na utawala wa Mikoa, kutokea ma PC mpaka hadi Chief, serikali ya Katiba ile nimeona kama kwamba ime enda makosa, kulingana na Katiba hiyo ya zamani. Ingelifaa, kwa maoni yangu, ingelifaa wale ma chiefu wa Kenya nzima iwe kwa namna mbili, ima wawe kuchaguliwa na wananchi kama wa councillors na wabunge.

Pili, wawe ni wenye kwenda yani transfer, kama wale ma DO na ma DC na ma PC. Kwa sababu niki fefenua, tunaona kama nafasi hii itakosekana kwa hawa ma chief, ikiwa chief si mwenye maendeleo, kwa vile amechaguliwa na serikali, ikiwa chief si mwenye maendeleo, mutabaki na yeye mpaka ile miaka ambaye ata retire, hata kama ni miaka hamsini, hamuna kitu ambayo munajengeka. Lakini, kama kuwa atakua na nafasi ya transfer, itakua chief yule ni mwenye kuja kama DO kisha aende tumpate mwingine ambaye ana maendeleo, ambawo atatujenga kuliko yule ambaye atakaa hapo na akeye hapo milele. Kwa hivyo kwa Katiba hii mpya, naomba, ili ma chief wawe na nafasi, yani wananchi wawe na nafasi, machiefu wawe ni wenye kuwa kuchaguliwa na wananchi ama hata kama si wananchi kuwachugua lakini wawe na wakati wa kuenda, locations zingine. Mchango wangu wa kwanza huwo.

Wa pili, kulingana na Katiba ile na serikali ile, wamesema, serikali wamesema kuna uhuru wa kuabudu, dini zote kuna uhuru wa kuabudu. Lakini tunaona katika jambo hilo, halikua la kweli. Kwa sababu utakuta ziko dini nyingi ambawo yani ma dhehebu yawo mategemeya Jumapili, Ijumaa, Jumamosi, Jumapili. Lakini Ijumaa na Jumamosi utaona haikutambuliwa. Ilitambuliwa Jumapili peke yake, ambawo Waisilamu, Ijumaa ndiyo siku yawo ya mapumuziko na kumtambua Mungu kwa kulingana na mapumuziko yawo. Haikutaja, haikuwaruhusu hiyo Ijumaa kuitambua kama siku yawo ha holiday. Kwa hivyo kwa Katiba hii mpya ya sasa mimi natoa mapendekezo yale madhehebu ambayo yamekua Ijumaa, yawo ni Ijumaa na Jumamosi na Jumapili, serikali itenge hizo siku tatu yale madhehebu kama hayo, madini kama hayo yaweze kupata nafasi hiyo.

Jambo la mwisho, mimi napendekeza katika katiba hii, wale wageni ambawo watakua niwenye kutoka nchi zingine na kuingia nchi hii, kuchukuwa uraia wa Kenya, serikali kwa Katiba hii, isiwakubalie kama vile hiyo Katiba ya zamani au serikali hiyo. Kwa sababu, tumegunduwa ya kwamba kulingana na nafasi hiyo, kuna kabila zingine kule wanakotoka, kupigana au kugombana, kuwa ni jambo la kawaida kama kukata nyele, yani kupigana mabunduki au kuuwana, ni jambo la kawaida kama kukata nyele tu au vile Masai kukata sikio. Sasa kwa sababu kwa kupatia nafasi hiyo ya watu kama hawo, kuwa wata kubaliwa kuja kwa wengine ambawo hawana tabia kama hiyo, labda tumeona ndiyo inachangia watu wengine kugombana ambawo kutokea mababu na mababu wanaishi bila mgombano. Kama vile wa Pokomo na wa Orma. Kwa sababu kama ni wale wengine wanasema ati ni kwa ajili kutetea mtotana maji, au mashamba, ni urongo si ukweli hiyo. Kutokea zamani mababu na mababu, mu Orma ngombe anazo, mu Pokomo, mashamba anayo, na hakuna ngome aliekufa kwa sababu ya kukosa maji, na hakuna mu Pokomo aliokosa shamba, kwa hivyo, hawa wameelewa, hawa ni wachocheaji kwa kutoka hawa watu wawili waendelee kugombana. Kwa hivyo kusema hivyo, Katiba hii ya sasa, iwakoseshe nafasi watu kama hawo, napendelea kwamba ili watu kama hawo ikiwa watakuja, kuwa wapewe uraia ya Kenya, iangaliwe sehemu ambayo itakua wale makabila wanaoishi kutokea mababu na mababu, iwatengwe sehemu ambawo ziko hii Kenya, ziko hii Kenya, sehemu ambawo zina

kuwa hazina watu. Hawa watu wawe ni wenye kupewa hizo sehemu waishi kuliko hivi sasa vilivyo ambawo wanachanganywa tuko wale wengine kisha wanalete kasuba mbaya kama wa Pokomo vile tulivo ona wa Pokomo na wa Orma.

**Com. Maranga –** Asante Bw. Dawa. Nimesema asante.

**Bw. Dawa –** Nimekomea hapo. Ndiyo.

**Com. Maranga –** Nimesema asante. Na utuweke kitabu chetu sahihi na nashukuru sana kwa maoni yako. Mwingine anayefuata ni Ali Jubo. Ali Jubo. Sijui ni Jubo au Jubu

**Ali Jubo –** Asalamaleikum

**Com. Maranga –** Majina kamili mzee.

**Ali Jubo –** Ali Jubo. Mkaaji wa Tana River.

**Com. Maranga –** Endelea

**Ali Jubo –** Mimi sina mengi. Lakini kitu kina tushangaza kwa serikali yetu tukufu, sisi tulipo fungua macho kutoka mkoloni vita vya Italian na Mwingereza, twaviangalia hivi, hatu kuona mengi yapo yalio zuka sasa hivi. Tume muona mwingereza ameketi na sisi akielewa kama hawa ni raia zangu, mfano hakumuonea tu. Lakini tumekuja kusema sisi tupate uhuru wetu tutatokana na mazito, hivi sasa ndiyo mazito yametuingilia. Sababu mwingereza ametoa wajukumu la kila mutu aketi pale pake aliopo alipo zaliwa. Aki ingilia kwa mwenzake, aingiye kwa amuri ya serikali. Lakini sasa tumeone mukorogano umeingia, na balaa zime tuingilia, kwa mfano, mu Pokoko hajui vita vya wowote kugombana na mtu. Mu Pokomo ndiyo mjinga kabisa ambaye hashiriki mambo ya vita. Mwaona sasa kwa kuwa sasa Mupokomo ndiyo aliofanywa, baada ya kuchokozwa, aliofanywa ndiye mchokozi, baada ya kuendewe vijijini kwake na kuvamiwa, na kuwawa imekuwa hawezi kukataa, ni kuwacha tu awawe. Hii ni jambo la ajabu. Sisi hatukuwa na imani ya serikali kama hii, wafahamu?

Pili, kama mutu amesema mazingira, mazingira, sisi Wapokomo, na Tana River, tunawo mazingira ya majaabu.bila licence. Tumeketi sisi, Ndovu alikuja mjini tele kwa tele mashamba, kikoma saa kumi na mbili, uwezi ukaingia. Tulipo pata uhuru, tumewacha Ndovu wakaingia wageni kuwauwa Ndovu kama kuku. Na hali ndiyo store ya Kenya nzima. Wa fahamu? Na ukienda kupigia report kwa kuwa Ndovu huku huwawa, hiyo serikali itakuja kwa siku ya pili ama siki ya tatu akuulize, wale wajambazi waliouwa hawa wanyama wako wapi? Yule ni mgonjwa uuwa wanyama ni ule pale. Na tena akuambie wewe uliokuja ku sema ndiyo humupa chakula kila kitu. Na wewe hujuta kwa chakula kule kwako, huuja na mbuduki zake na kila kitu, ukiwambia toa chakula unipe. Utampa wewe? Lakini umeonekana kama sisi ndiyo twafuga wanyama. Je sasa wageni

wame chukua store Tana River ya Kenya mzima, ndiyo tumekua masikini kabisa. Sasa mwasema mazingira, mazingira, mazingira yako wapi sasa. Haru, hakuna. Ndovu hakuna, ndiyo zetu store ya Tana River, ya Kenya. Tuko wapi? Na tukihadhara tu ya kwamba hakuna serikali, serikali ikikoma wale, wale serikali. Ukipewa shamba na Kamati, chief awezi akaaja akachukuwa akampa mutu mwingine. Kamati imetowa (haina fahamu hii) na akakuambia wewe nimechukua shamba yako nikampa huyu, utafanya nini? Angalia, iko serious kitu gani ukifikiria? Ndiyo serikali, ukikoma, ukikoma la pili kabisa, ukitaka kufungua macho yetu, natukielewa, Chief utolewa na raia. Haa sub-chief kuende kufanyiwa interview. Hii interview, ni kuongoza ama yarifa masomo? Hatu kuona kama mutu ati interview ndiyo akili ya kuzaliwa. Ume fahamu. Wewe unachukua nyoka unamlete kwa interview alafu sisi tufanye nini, ata tuuma tu. Sasa raia wataka, mwanzo chief mpaka sub-chief, mpaka DC, mpaka DO tufanye kama kawaida, atolewe na raia. Lakini tunaona maumivu juu letu. Angalia basi, wamsema serikali mutu akiliwa mali yake atalipwa, umeona? Sasa hivi wanyama huwa ndiyo waalia watu, na ukienda kwa Game ukitoa report, ya kwamba wanyama huku watusumbua, hata habari hawana. Habari hawana. Ebu, muuwe panya sasa hivi, muuwe panya, utaajiwa na kikosi kizima. Kuja kuhojiwa wewe, Ni haki? Ndiyo haki, ndiyo ukweli? Na akiila nyama huna malipo jana wala usiku. Mimi hali hii, nimsomeshe na nini mwanangu? Na elimu imewekwa kwa wale wenye mapesa sasa. Imewekwa kwa wale wenya mapesa. Maskini hajulikani kwa masomo. Umenambia peleke mtoto wako skuli, ni msomeshe na nini? Kwa hivo sisi twataka jukumu hili lirudi kwa raia. Wachagwe wenyewe. DC utoka hapa akitaka kutoa chief, huleta, jumatatu naaja. Asije akasema mimi napita huku, mzee munipe Chief.

**Com. Maranga –** Asante mze wangu. Ongea kwa ile machine. Asante mzee wangu.

**Mzee Jubo–** Mzee munipe chiefu, akitokea, akija kutoka, chief uko wapi mzee? Wafahamu. Kwanza Kuanzia kwambia chief ni huyu, sababu kijiji hiki kizima hiki Kipini, wajua kila mtoto akili yake. Huyu ni mbaya, huyu ni mzuri, mpaka akagundua, waka kute yule mtoto ambaye aweze kuasaidia. Sasa useme nitakwenda kwa interview, interview uchukuliwa na nini? Elimu ni kuongeza marifa. Elimu ni kuongeza marifa, sio akili ya kuzaliwa.

**Com. Maranga –** Asante mzee. Ume maliza?

**Mzee Jubo –** Nimemaliza baba.

**Com. Maranga –** Samahani. Asante. Basi tuweke sahihi kitabe chetu rasmi, na nashukuru kwa maoni yako. Asante. Pita pande hii. Yule mwingine anaye fuata ni Mahasan Abdulrahman. Wapi? Ni wewe? Haya una dakika chache kabisa. Ni wewe? Wapi Mahasan. Mahaseni Abdulrahman. Hayuko. Haya tuje kwa Kombo Eliza? Kombo? Dakika chache kabisa. Yule mzee tulimuheshimu ndiyo akaelekea kabisa.

**Kombo Eliza –** Hakuna wasi wasi. Asante sana. Mimi Kwa jina naitwa Kombo Eliza. Nimukaaji ya Ozi, Mpeketoni. Maoni yangu wa kuchangia ya leo katika hii Katiba mpya ni upande wa mume na mwanamke. Kwa sababu unakuta pengine ndugu

yako yuko na kazi na wame zaa watoto, na huja Mwenyezi Mungu akaleta rehema zake, alafu yule bwana akafa, na ile pesa ambawo imebakia kwa upande ule wa kazi, inatakiwa yule ndugu yake hana haki kuenda kupata ni mpaka yule mwanamuke achukuwe, na ukiangalia ile dhamana ya wale watoto ni huyu ndugu yake. Kwa upande wa Katiba, serikali iangalie vizuri.

Na lingine nikusema upande ule wa ma Headmen. Ma Headmen ndiyo wana fanya kazi kulingamana na kazi za serikali za hapa nchini Kenya. Ni kwa sababu gani wakatu ule ma mukoloni ambapo waliakua wakipata hata kama ni shilingi moja? Leo imekuwa wa Kenya huru, iwe Headman hana kitu chochote. Anamutumikiya Assistant Chief, anamutumikiya DO, anamutumikiya DC, mpaka Mombasa, kule kwa PC mpka kwa Rais, ni kwanini akose kitu kidogo?

Tatu ni kusema kwamba, turudi upande wa ardhi. Ni kwa nini baba yangu alishika upanga aka fieka msitu, alafu akawowa mama, nikazaliwa hapo, na baba yake alikua hapo, na mimi nikakua na hiyo mahala, leo mutu ambawo anaishi Ulaya, atoke huko, yani aje achukuwe hio mahali inaonekana kwamba hakuna haki yoyote yakivinadamu ambapo atanyanyasha huyu mutu. Hakuna haki yotote ambayo inaweza kupitika yani, huyu mutu, yani anyakuliwe ile ardhi.

Ingine ni kusema kwamba upande mwingine tukiongezea yani, upande wa wanyama, umekaminika, upande wa wanyama na vinadamu, yani munyama ana thamani zaidi. Wote waliumbua na Mwenyezi Mungu, lakini kwanini ule ali itwa mnyama na ule ali itwa binadamu? Wako na tafauti. Imekuwa serikali ya leo imechukuwa mnyama na binaadam naye binaadam mwenyewe ambawo analima na kutoa afia imekua ile mnyama ana, yani ile thamani yake inazidi kwa upande wa serikali, kwa sababu kwa upande wa serikali ule mnyama anaweka pesa zakitalii ama wageni tofauti fotauti. Kwa hivyo maoni yangu ningependelea kwa kurebisha Katiba, hii maneno iangaliwe vizuri.

**Com. Maranga –** Nashukuru. Weka sahihi kitabu chetu rasmi.

**Kombo Eliza** - Asante.

**Com. Maranga** - Nashukuru kwa maoni yako. Muhamed Omar Dado? Wakati ni wako.

**Muhamed Omar Dado –** Salamaleikum. Mimi jina langu naitwa Muhamed Omar Dado. Na mimi kitu cha kwanza ambacho nitachangia ni habari ya matibabu ya hospitali. Serikali ya leo au Katiba ya juzi na jana, mpaka leo ni kwamba serikali imekubali kuumia raia waafilie mbali waondoke kubakie mapesa. Sababu kusungumuza hivi ni kwamba daktari mwenyewe anapanga hospitali anaweka, madawa ananunua wapi? Huyu daktari anapanga hospitali yake mwenyewe, anapanga anaiweka. Madawa hupata wapi? Madawa hupata kupambanya kwa sababu kuuumiza wananchi, yeye apate kunufaika, na serikali yetu imekubali. Sasa basi, yani kupeyana mawazo au kuchangiana mawazo mimi nataka hivi, serekali ifanye biddi kuhusika na habari ya matibabu ya rudi kama namna ya zamani ambayo kwamba yaliokweko. Sababu wananchi wanaumia wengi. Ilo ni kitu chakuanza kumemalizika.

Maswala ya Ardhi, tunanyanga'nywa ardhi hasua wa Tana River, yani kiholela. Kwa sababu imeonekanwa ardhi, nawenyewe ni wanyonge. Kwa sababu ya kufanywa wanyonge, sasa ni ya ardhi tuchukuwe tu sisi ambawo kwamba tuko na nguvu. Sababu ya sungumuza hivi, nyumba yake hii umeijenga, unaishi wewe hii nyumba ni yako. Halafu mutu kutoka Kisumu, au kutoka India, ainunuwe nyumba hii na nyumba hii anaekaa ni wewe. Hiyo sio haki. Sababu yule ambaye kwamba ni mzaliwa wa hapa, ni muzaliwa wa hapo, ambawo kwamba amezaliwa hapo, babu, babu mpaka baba, atoke mutu kutoka Nairobi, au atoke mutu kutoka India, atoke mutu kutoka America, awe yeye yuko ana haki zaidi kunishinda mimi ambaye kwamba nimekaa hapa, kisha kinyume kinasungumuzwa lugha yakustababisha, tunaitwa ma squartters. Yule ambaye amenunua, akatoa pesa, hakuwe squarter, squarter itakuwa ni mimi.

Kwa hivyo sasa twapenda serikali kulingamana ni hiyo Katiba, sisi tuma squarters, sisi tuna kwetu kweli, ardhi ni wetu. Kuhusika na mambo ya ardhi, ipitie kwa wazee wa miji, ardhi kama ni mutu yoyote anayetoka kutoka huko, basi arudi aje aonane na wenyewe, kama ni Kipini, aonane na watu wa Kipini, kama ni Ozi, aonanane na watu wa Ozi, jumla Kenya nzima. Alafu aende akapate kila ambacho kwamba atakakipate huko. Lakini kuchukuwa mutu achukuwe hii Title Deed kutoka Nairobi, kisha shamba ni yangu, hiyo serikali ina tufanyia dhuluma, na ilikua ikitufanyia dhuluma sana. Kwa hivyo mimi napende kama yawezekana kuhusika na hiyo Katiba mpya, ambayo kwamba inapangwa, basi irudi hiyo ardhi yoyote ambaye ameichukuwa basi irudi ardhi kwa wananchi. Aliotoa pesa ambaye hakutoa pesa, ardhi siyake, ardhi ni wananchi wa Ozi, ni wananchi wa Kipini, ni wananchi wa Witu, Kenya nzima kwa jumla.

Kitu ambacho kwamba ilikua, nilikisubiri kwamba nitaona wenzangu hapa wakisungumuza, lakini sijui nawo kimewatoka, vichwani. Kitu ambacho, Kenya kina tusumbuwa, ni mutu ameuwa mutu, ana shikwa, anatiwa ndani. Alafu watu wanaenda kiholela, wanapewa pesa, kisha … anawachiliwa. Na ikiwa haki ya mtu, akiuwa mutu ni yeye awawe. Kwa nini mutu akiuwa mtu analipiwa pesa? Pesa zina thamani kuliko mutu? Pesa zina thamani kuliko mtu? Kwa hivyo twataka Katiba hii ya leo kama itapangika, ipangwe, basi ni mtu akiuwa mtu naye awawe bila case sababu akiuwa naye awawe. Basi.

**Com. Maranga –** Asante Mzee wangu. Malizia

**Mzee Omar Dado –** Nimalizie?

**Com. Maranga –** Yeah. Useme yako ya mwisho. Kama una memorandum unaweza ukatupatia. La mwisho.

**Omar Dado –** Kitu chengine kama ni la mwisho, nilikuwanayo sita, lakini haidhuru. Kitu kingine nitazungumuzia ardhi tumemaliza. Nitasungumuzia elimu. Elimu, kama alivyo sema, sijui ninani, elimu sasa sio ya masikini ni kuwachia wenye pesa wasome. Sababu vijana wengi, kama ni Kipini, kama ni Ozi, kama ni popote, kama ni Witu, kuendelea Kenya nzima, huwa watoto wanakuwa na akili wa kutosha ya kusomea na wapate masomo ya kikweli. Lakini kuajili ya kuomba baba, ni dhuaifu, yule mtoto apati masomo kisha tuna tukanua tuna ambiwa nyinyi amtaki kusomesha. Pesa ambazo kwamba zinatolea kusaidia

hama masikini ambawo kwamba nawo, watasomesha watoto wawe nikama watu, wamekanyagua. Kwa sababu wakisoma, watakuja ona mambo, watayakataa. Kwa hivyo kwa muda huu, serikali ifikirie sana kuhusika na hapa, ambapo pana husika pa elimu. Ifikirie na utufanyie musaada.

**Com. Maranga –** Asante. Basi nashukuru kwa maoni yako. Weka sahihi kitabu chetu rasmi. Mwingine ambaye namwita ni Samuel Haraka. Ako? Samual. Haya maoni ziwe dakika chache tu kwa sababu inaonekana watu ni wengi.

**Samuel Haraka –** Mimi kwa jina naitwa Samuel Haraka. Nimtaalam wa mambo ya baharini.. Mimi nafikiri nina mambo ma nne peke yake.

Jambo la kwanza ni kwamba, kwa sasa serikali yetu ya Kenya na wananchi hawana mafuta. Kila kiongozi anajua kwamba tunategemea kilimo. Na katika kilimo kuna sehemu tatu. Hizi sehemu tatu ni kwa upande wa mifugo, upande wa mimeya na upande wa viungo ambaye vime patikana ndani ya maji. Sasa unapata kwamba, katika Katiba yetu haisemi chochote. Sasa unapata yule Permanent Secretary, anapanga analetea wakulima mbegu, amepanga anapatia mutu mkopo wa kununua Tractor, anasahao kupatia mvuvi pesa za kwenda baharini, anasahao kupatie mvuvi (interjection)

**Com. Maranga –** Ongea kwa kibabi ya hio ndiyo tutasikia sauti.

**Samuel Haraka –** O.K. Wanasahao kupatia mvuvi pesa ajisadia anunue Troller. Kwa hivyo kwa upande mwingine, mimi tu nilikua nasema Katiba iwe wazi, kwamba wale wavuvi ambaye wanafanya kazi baharini wa angaliwe kama wale wakulima kwenya inchi kavu.

Na kwa upande mwingine nilikua napendekeza kwamba, katika Katiba yetu waweze kuazima ule mtindo ambawo inapatikana kule Tanzania. Tanzania, hizi meli ambazo zina vua hapa, hapa zina vua tatu wote na kelele, Tanzania Troller na ishirini, mwananinchi ananufaika, serikali ananufaika na matajiri wana nufaika. Kwa hivyo na omba, Katiba yetu iwe serikali iyazime huwo mtindo ambayo uko Tanzania.

Ingine ni hawa Watumishi wa Uma. Unapata kwamba Watumishi wengi Wauma, pengine unapata mwalimu, anasema mimi ni mihimu, daktari anasema mimi ni muhimu, mimi nilikua napendekeza kwa Katiba iseme ni Public Servant. Kwa mfano ni kama hivi, roho ndiyo inatupatia damu, je mdomo ikikataa kutafuna ama mkono ukikataa kupatia, kwa hivyo sasa wote waitwe Public Servant. Na kama mutu amesoma amefika kiwango cha Form Four, na yule mwingine amesoma amefika kiwango cha University, wote walipwe sawa

Kwa upande mwingine, nilikua nasema, kuna ile Kenya Gazette. Mutu anaenda Nairobi ana pipisha Kenya Gazette ile nyumba ni yangu. Kenya Gazette aipatikani kila mahali, na ni siku tisaini. Sasa mutu akisutuka hiyo nyumba ni ya yule mwenyewe.

Nilikuwa napendekesha ya kwamba, ile Kenya Gazette, iwe mutu kama ameenda kutaka nyumba, Kenya Gazette zizungushwe kwa ma chiefu, machiefu wazungushe kwenya baraza, watangaze mutu fulani anataka kitu fulani, ili ya kwamba mutu wowote asiweze kunyimwa haki.

Ingine ni kwamba hawa Wabunge wetu ambaye tunawachagua kwenda Parliament, ningependa kwamba, kuna ile sitting allowance, uko Parliament, mbunge ikiwa hakwenda Parliament, awe hana chake.

**Com. Maranga –** O.K. asante Bwana Haraka. Mwingine anaye fuata, asante kwa maoni yako, nashukuru, weka sahihi kitabu chetu rasmi. Mwingine anaye fuata ni Jacinta Mwangi. Jacinta? Mama una dakika chache tu utowe maoni ya muhimu.

**Jacinta Mugo –** Jina yangu naitwa Jacinta Mugo, mimi ni Mkikuyu. Na ninafurahi sana nikichangia Katiba ya leo. Kwa maana tangu tumepigania hii inchi yetu, nimeona kama miaka, tangu Mzee amefariki, Kenya yetu inaharibika. Kwa maana ule Rais yiko, amechukua jukumu kali, yeye ma office yote, kila offici funguo ni yake. Alisahawo ni wenye kupigana na msungu. Amesahawo ni watoto baba zao na wamama zao wamekufa kwa kupigana na mzungu. Ile ardhi tumepiganiya leo hii ni ya mzungu. Mwingeresa ameingia Kenya. Mwarabu ameingia Kenya, ni uhuru gani tumepigania miaka saba imepita?

Kwa Katiba ya leo, mimi nikichangia, ule Raisi atakua mwaka hii tutaenda, akuwe yeye chini ya wananchi. Sio kuchukuwa ufunguo, anataka kwenda ngambo, anachukuwa wazungu analete hapa. Anaenda huko inchi ya Warabu, analeta Warabu hapa. Anaenda kila inchi ingine, analete watu wa pande ingine hapa. Tumepigania uhuru tukiweka Katiba moja, sisi Wakikuyu, tuka sema katika Kenya, pembe nne, mutu nyeusi, sisi hakuna ukabila, lakini mutu nyeupe hamutaki area yetu. Alitulalia miaka sabini. Tangu Mzee amekufa, sijui ni miaka ishiri, ime rudi ile ile tu ya mwanzo. Huyu Raisi, namjua yeye anapende kulete watu wa nchi ingine, kwa maana hata yeye si muzaliwa wa Kenya. Ndiyo wanataka sasa watu wa inchi wengine waingie hapa. Mimi sikusema kwa kudhuru yeye. Tangu pahali alizaliwa, na mimi nilizaliwa, hapo hapo Rift Valley. Mimi namjua kweli, niki ingia musituni, nilikuwa musichana wa miaka kumi na sita. Ni kusema Katiba ..

**Com. Maranga –** Mama nataka ujirekebishe kidogo, sisi hapa kama Tume ya kurekebisha Katiba, hatukubali kusungumuzia mutu binafsi. Unazungumuzya offici, kama Office ya DO, kama ni ya President, unazungumuzia offici, sio mutu binafsi.

**Jacinta Mugo –** Haya. Kama ni hivyo ule Rais atakalia kiti akuwe chini yetu. Na aondoe wazungu area yetu ya Kenya pembe nne, na aondoe Muhindi, anatunyonyesha mali yetu yote ina tumiwa na Muindi. Aondoe hawa. Tunataka watu wa Kenya, raia wa Kenya, tukuwe sisi naye iko na kibali ya kuuza mali yetu. Kama kupeleka Ulaya, kupeleka inchi zingine, tukuwe ni sisi wenyewe. Lakini si kufuatia matajiri wanaendelea hapa Kenya yetu si ya kufurahisha. Hiyo ni ya kupiganisha wananchi. Tuna kosa imani.

Kitu inaitwa majimbo. Majimbo ndiyo tulipigana naye na mzungu. Na tukaweka sign Katiba kama hii. Hatutaki majimbo katika Kenya. Na sasa hii majimbo ndiyo inalete ukabila. Yangu ni hiyo tu.

**Com. Maranga –** Basi asante mama. Thank you very much. Tuwekee sahihi kitabu chetu. Asante kwa maoni yako. Mwingine ni John Ngige. John Ngige? Hayuko? Oh, John Ngige. Haya. Utoe kwa ufupi kabisa. Saa ndiyo hizo ina yoyoma. John Ngige.

**John Ngige –** Jina langu ni John Ngige. Nimukulima wa hapa. Maoni yangu kuhusu kuchangia Katiba hii mpya, nita anza na miundo ya serikali. Katika Kenya, tangu mwamzo tumekuwa na rais na makamo wake. Na Katiba ambayo wakati huu mimi ningeuliza, ama ninge sema kwa maoni yangu ya kwamba, kuwe na Waziri Mkuu, kwa sababu naona Rais ana hangaika sana. Kama ni Show kufungua ni rais, kufungua kiwanja ni rais, kwenda hotel ni rais, kwa hivo, kukiwa na Waziri Mkuu, atamusaidia kazi kidogo. Na ile Waziri Mkuu, ni kutokana na ule upigaji wa kura. Maana Kenya yetu ina chama nyingi. Ile chama ya pili, waziri mkuu anaweza kutoka pale. Hapo nimetoka.

Ninaenda kwa upande wa kilimo. Mimi ni mukulima. Jambo ambalo ningeomba Katiba ya sasa, tangu mwanzo wakati tulikuwa na Mwingereza, na baada na Mwingeraza tukawa na Marehemu Rais Kenyattaa, kulikuwa na mshirika mengi ya serikali ambayo ilikua inaitua, KFA, hata wakati wa juzi, juzi tulikuwa na NIP, wengine walikua wanaitwa Cotton Lint, nakusema ukweli, kitu kime kiaribu hapa ni soko huru. Hii soko huru imetuumiza sana, na sijui hii Katiba ilitoka wapi, maana kulikuwa na mashirika mengi ya kutusaidia. Soko huru hii, juzi tumepata mbegu hapa, serikali imeleta mbegu. Mbegu wamelete, lakini kuja kujua ile kitu imetoma pale inaenda wapi, hawakuji. Ni mutu tu anakuja tu anasema nitanunua pamba shillingi kumi na tano. Kama hamtaki, mimi naenda. Hakuna mutu ya kusema, hakuna mutu ya kuzungumuza.
Kuna Wabunge, kuna wengine ambawo ni Macouncillors, lakini tunaona ya kwamba wakati wa yule mutu kuja kununua kwa sababu ni soko huru, uwezi kumwona mbunge au councilor ama yoyote. Ni wewe na mwenye kununua. Pale, sababu ya shida zako, mtoto yako yuko hapo unataka aende shule, unaona ya kwamba utawuza ile kumi na tano. Hapo, mimi ninge omba ya kwamba, Katiba ya leo kuwe na mumunuzi vizuri, kuwe tukitafutiwa mununuzi vizuri wa ukweli, kwa sababu tukiwachiwa mimi na mwenya kununua, tuna umia sana. Hapa watoto wetu wengi hawasomi, kwa sababu ya hiyo soko huru. Unatoa kidogo, na imeuzwa na huna njia ingine ya kupeleka.

Jambo lingine, ni kuhusu uhaki kwa wanaume. Wanaume ningeomba ya kwamba kume kuwa na shida katika sisi, kwa sababu unapo endelea kusikiza Radio na mambo mengine, unakuta ya kwamba mwanaume hana haki. Mwanaume ana bibi, ana mtoto. Mtoto yule anaweza kuwa mutukutu. Hataki kusoma, hataki kufanya kazi ya nyumbani. Ukienda umshike, ama umwambiye sababu ufanyi kazi hapa kwangu sikutaki, anakwambia, haki yangu ni kwamba, lazima unipe. Kama yule mtoto awezi kulima, sasa nitampa nini? Ukimuchukua ama umufukuze, ana enda kwa DO, anaend Polisi, mzee anachukuliwa mapingo mkononi, mbona unamusumbua mtoto, hakuna haki ya mzee, mzee anawekwa ndani, shamba inagawanywa huku, mzee mwingine aliamwambiwa pale, mpake ukubali mtoto agawanyiwe. Mtoto anasema mimi nataka mbuzi mbili, na acre mbili,

mzee sababu amefungua huko na amefinywa, shamba inagawanywa. Asante.

**Com. Maranga** – Asante. Haya anza na majina yako.

**Veronica Kwamboka** – Kwa majina yangu, naitwa Veronica Kwamboka. Nimkaaji wa Kiswilani, hapa Kipini Division. Maoni yangu, nina maoni ma tatu, ingawaji pia yamesha sungumuzwa na watu, lakini ningependa kuongezea.

Maoni yangu ya kwanza juu ya Katiba yetu ya Kenya, ni kuhusu Afya ya wananchi. Sipitali zetu za Kenya kutoka mwanzo tulikuwa tukitibiwa bure. Lakini sasa imekua ni pesa na hali ya uchumi ya wananchi wakulima iko chini sana. Kusema ukweli ni kwamba, tuna lima, tuna vuna, lakini mavuno yetu hayana faida. Tunauza kwa beyi ya chini. Tukiangalia hospitalini tunalipishwa beyi kali. Tunaweza kuwa mtu ni mgonjwa, lakini pesa za kutibu yule mtu unakosa. Mtu anaumia pale ndani ya nyumba kwa ajili ya kukosa mapato.

Jambo la pili, ni kuhusu Ardhi. Tunao mashamba, wananchi tume kaa tunajua kwamba tume kaa katika Kenya tukiwa na uhuru wa kulima mashamba, lakini hatuna Title Deed. Tutajuaje kwamba sisi ni wana Kenya, natuna mashamba, ikiwa kama hatuna Title Deed ya kuonyesha kwamba tuna ma shamba? Na tuta juane kwamba yale mashamba ni yetu? Ningeomba serikali yetu, ikapate kulichukuwa hili jukumu kupitia kwa Katiba.

Jambo la tatu ni kuhusu Elimu. Ningeomba kwamba serikali yetu ingepata kutupatia elimu ya bure kwanzia darasa la kwanza mpaka darasa la nane. Kwa sababu ya hali ya mazingira ya wananchi. Yangu ni hayo asante.

**Com. Maranga** – Asante Bi.Kwamboka na asante kwa maoni yako, weka sahihi kwa kitabu chetu rasmi na nimepiga asante sana. Basi kwa niaba ya Tume ya Kurekebisha Katiba, tunaelewa ya kuwa hapa area hii, lazima turudi hadi Malindi ndiyo tuweze tukarudi ndiyo kesho tuende Garsen, tena pande ingine Garsen, kwa hivyo ningeomba tu wananchi nataka kuwashukuru kwa niaba ya Tume ya Kurekebisha Katiba, na sisi kama wana Tume, wale ambawo wananchi waliojiandikisha, wote wame toa maoni, na hii maoni yenu, tutayatilia manani na report itarudi hapa hapa, mutakuja kuisoma ili mujuwe kama ile maoni muli toa kweli hii Tume ya Kurekebisha Katiba imeweka kwa hali nzuri. Tunaelewana kwa hiyo maneno? Kwa hivyo mimi nataka kupiga asante sana, lakini hatujamaliza kabisa, ningeomba tu Bwana Co-ordinator, uwe kama una machache yakusungumizia ili tuweze tuka maliza na maombi ya Mwenyezi Mungu. Asante sana.

**Co-ordinator** – Wamejitaidi wamefika mpaka kwenu, na wamepokea maoni yenu, nawashukuru sana. Ningependa pia kuwashukuru wananchi kwa kujitolea, najua mumetoka sehemu mbali, mbali, mukatumia midawo, wengine wakatembeya, lakini mukajikakamua mukafika mukutano wa leo, na hii ni kwa sababu mume elewa umihimu wa Katiba ambawo inatengenezwa ambayo Katiba ndiyo uti wa mgongo wa maisha ya kila Mkenya. Ningependa sasa bila kutumia maneno zaidi, kwa sababu wageni wetu wangependa kwenda mpaka Malindi, ingawa tunawaomba wakija, wajitahidi kutumia vifaa ambavyo tuko navyo,

tuko na vifaa vizuri sana sehemu ya Garsen, ambapo mukilala, mutajikuta muko kama Nairobi na Mombasa, nakule Malindi munako enda, natutawaonesha mfano Mzee Islam ametoa Hoteli yake ili kwa kirimu wageni wetu kwa mangkuli ya lunch, na wakienda hapo, nafikiri watapa penda na siku zijazo, mukija kwetu, muje muwe wageni wetu kabisa. Si wananchi munge penda hivyo?

Majibu – Sana.

**Co-ordinator** – Basi. Sasa, tumechukuwa muda mwingi, tumeteneneza chakula. Ilo ndilo ambalo tungeweza kwa sababu tume hurumia wale walio toka mbali. Kwa hivyo wananchi na kila ambaye kwamba yuko hapa, chakula imetengenezwa, Chiefu yuko, na Councillor yuko, wataone vile ambavyo mutapata mangkuli, ndipo muwe kutembeya mpaka muliko toka. Na wageni wetu watakurimiwa kule kwa hoteli, kwa hivyo wale wananchi wabaki hapa, tupate viongozi wa chache, twende nawo kule, ili waweze kujumwika na ma Commissioners wakajadiliana mambo mawili matatu. Na basi kwa ajili ya kufunga mukutano natoa shukuruna kwa kila mmoja alie kuja hapa, ningependa sasa kumwalika Rev. Bagaja Keya wa Kanisa la Methodist aje atufungie kwa maombi, Mwenyezi Mungu ambariki kila mmoja, asanteni.

**Rev. Bagaja Keya** – Natuombe. Katika Jina la Yesu eh Mungu, tunasema ni asante, tazama vile umetufikisha na vile tumeshirikiana, tukakubaliana na yote ambayo tumekwisha ya fanya. Tunakuomba sana Eh Mungu, uingie na ukamilishe pale tumeibakisha na ukamilisha na kujaza zaidi sana kuondoa unyonge na kutupatia nguvu na ustawi na ushindi katika nchi yetu. Na hata wageni, uwape safari ya kurudi salama, mpaka tuonane tena kwa Utukufu wako, Amen.

**Speaker** - Kutoka Ozi. Maoni yangu ni kuhusu Watumishi wa Uma. Ikiwa ni mutumishi wa serikali hasa wangazi wa DO ama wa DC ama wa PC, akipatikana na kashfa, ya uovu, ikiwa ni kuhusu vita, pesa ama uharibifu wowote badala ya kuondolewe transfer kupelekwa kwingine, awe afutwe kazi. Na kuhusu shuhuli ya uhifadhi badala ya kutafuta kwa andika ma officers ambawo wana kaa Nairobi na Mombasa, na misitu yetu, mali yetu yana ngamia hapa, ile pesa ya serikali iajiri hawa wenyeji katika yale maeneo ambapo huifadhi huko iwe, yale mapato yatakao lipwa wale vijana ambawo wameajiriwa kuifanya huwo uifadhi, iwe watajiendeleza ki maisha na ule uifadhi uendelee kuliko kuajiri mutu ambaye anakaa Nairobi na mshahara anakula na hakuna kitu kinafanyika.

Na kuhusu neno langu la nne ni kwamba serikali uwa una watumishi makubwa, makubwa kama ma PS's na wengineo, na hawa watu badala kuwa wanalipwa pesa na serikali, huwa watijimudu ki maisha na shuhuli zao zote, serikali huwa umewapingia pia matumizi ya kuwanunuliwa ma kochi, masufuria , kila kitu wana wawekea ndani ya nyumba ikiwa hawa watu wanalipwa mshahara na serikali. Badala yakumwacha huu masikini, badala ya kumlipa mshahara ili ile pesa anawo fanyia matumishi yake ya nyumbani, wamsaidie yule masikini, ambaye ajiwezi, wawo wanamutengeze nyumba yake, wanampambia kila kitu, ambapo zile pesa zina hudumia hawa watumishi wote wauma, zimekua zimesaidia masikini ama hawa wengine ambawo hawawezi kuelimisha watoto wawo, huwa hawo watoto wanabaki bila elimu, wale bado wanalipwa mshahara na pia bado wanaendelea kupambiwa manyumba wawo. Katika Katiba hii hili neno liangaliwe. Ni afadhali alipiwe tu ule mshahara asipambiwe nyumba yake.

Na kitu cha nne, cha mwisho, ni kwamba hawa watumishi wa watu wa Game. Hawa watu, ni lazima katika Katiba waangaliwe, kwa maana, hawa huwa ni rahisi kwenda kumpiga mutu, kuliko kwenda kumelimisha ili amhifadhi ile mnyama kwa manufaa ya wote wawili. Ni mara nyinya tumeshaa shirikiana na hawa watu, kuje kirahishi kama wame sikia mnyama wawo amewawa kuliko mnyama wawo ameuwa mutu au ameharibu mali. Sasa hawa watu wana uwaadui baina ya raia na wanyama. Ni vipi hawa watu wame elimisha watu, hawa wananchi wamelimishwa siku nyingi kufanyiwa mambo ya uifadhi ama kuwalinda wanyama, leo hawa wananchi wame elimika wanataka kumuifadhi hiyu mnyama, yeye mutu wa Game bado ana lile jukumu lakumfanyia huyu raia awe ni adui wa yule mnyama.

**Com. Maranga** – Asante.

**Speaker** - Kufikia hapo ni mwisho.

**Com. Maranga** – Asante sana. Nashukuru sana …… Tuwekee sahihi kitabu chetu rasmi Mwingine ambaye ninaye muita ni Abaye Eskofa. Abaye Eskofa, kuingia? Eskofa? Nafasi ni yako

**Abaye Eskofa** – Kwa majina minaitwa Abaye Eskofa

**Com. Marange –** Sauti kidogo?

**Abaye Eskofa –** Mkaji wa Kilelengwani ambaye mimi ni Mwalimu, kwa upande wa watu wazima. Yangu maoni ambawo kwamba niko nayo ni matatu na ni yale ya muhimu sana.

Jambo la kwanza ni usongamano wa magereza ambapo tuna magereza machache sana humu Tana River. Kwa hivyo tunaomba serekali pia ijaribu kupanua magereza katika sehemu ya Tana River.

Jambo la pili, serikali imeanzisha tangu zamani elimu ya watu wazima.

**Com. Maranga –** Tafadhalini mupe nafasi atoa maoni.

**Abaye Eskofa –** Lakini ainzingatii elimi hii serikali aishuhuliki. Imewachia wananche wenyeye na hatujui kwamba wale walimu ambawo kwamba wanahusika na sehemu hiyo wataindelezaje. Kwa hivyo tunaomba serikali pia isaidia kwa ujenzi kwa madarasa ambayo kwamba masomo haya yataendelea. Alafu vile vile, ijaribu kuchunguza mishahara ya walimu, ambawo kwamba wanasimamia elimu hiyo.

Jambo la tatu kuhusukana na sehemu hiyo ama kifungu hicho cha elimu, ni kwamba, waalimu ambawo kwamba waajiriwa na serikali, tunaona kwamba kuna ubaguzi ndani yake. Kuna waalimu ambawo kwamba wanaitwa part time teachers, na wale full time teachers, ikiwa wote ni waalimu, kwa tuna omba pia serikali ebu ijaribe kuwaweka sawa waalimu hawo. Awasadie na vitambulishe ili waweze kutambulika zaidi.

Jambo la tatu, modification of Courts. Mahakama yani. Katika Tana River yetu tuko na Court moja tu peke yake ambayo kwamba iko Hola. Kwa hivyo tunakuta kwamba mhalifu akishikwa hapa anaumizwa, kukotwa na pingu, gari inatikitishwa huku na huku, raia naumia kupelekwa mpaka hadi Hola, hana njia kwamba anaweza kujisaidia akashika mahali, raia wanaumia sana, wanaonewa. Kwa hivyo tunaomba pia iongezwe Mahakama katika Wilaya ya Tana River.

Jambo la nne, tunaomba heshima iwekwe kati ya polisi na raia. Polisi kumshika raia kwenda kumweka Cell, unaogelea mikojo wewe raia, ikiwa tayari kuna dini zingine ambazo kwamba airuhusu wewe kuogelea ile mkojo, lakini unatembelea ile mikojo, ambawo kwamba inakufikia goti ati waenda kukojoa huko. Pia Cell hizo ambazo kwamba tunawekwa, sisi raia tunaumizwa, serikali ichunguze, swala hilo ambalo kwamba tunanyanyaswa nalo katika polisi wetu.

Jambo la (nne), la mwisho ambalo kwamba mini ningependa kulizungumuzia, ni kuhusikana na mambo ya ardhi, hili jambo watu huja kuligonga gonga hapa, lakini hawaja lifafanua vizuri. Huku kuingiliana mufugaji na mukulima, hilo jambo ambalo kwamba limeleta ugomvi huu Tana River mwetu, kwa hivyo tunaomba katika Katiba ya leo serikali ijaribu kuwatengea ardhi wafugaji,

kisha iwapatie mutambo ambawo wangezeza kukamulia maziwa yawo na kuyatia katika ma mbomba ama packet, kisha biashara iweko ambawo ingeweza kujiendeleza wawo wenyewe badala ya kuchanganyikana alafu ngombe inaenda kwa shamba ya mtu, anaekula na maziwa unawiziwa. Hiyo pia ni jambo ambalo kwamba tunalijaribu kuitetea katika Tana River na serikali itusaidie. Asanteni.

**Com. Maranga** – Asante Bw. Eskofa. Sasa nakuomba uweke sahihi kitabu chetu rasmi. Mwingine ni Ali Amesa. Ali? Hayuko? Ako? Ali Amesa, hayuko? Sawa tu tumpite. Haya mwingine, kama huna maoni, huna maoni. Asante, asante. Yaya Maimuna Abdalla? Maimuna? Maimuna Abdalla?

**Maimuna Omari Abdalla** – Mimi jina langu naitwa Maimuna Omari Abdalla Headman, kutoka Kipini na nasema maneno ya kuhusu mambo ya Vijana kusomeshwa shule na wasichana, tuna umizwa sana na sisi tunafanya jitihadi za kutosha, kwa wasomesha watoto wasichana. Msichana akipelekwa shule anapata mimba, akawa ni hasomi tena, pengine yuko Form II, yuko Form I, yuko Form III, mtoto hana tena masomo. Kwa hivyo hili neno nataka lichukuliwe katika hili Katiba iwe ule ataekuku haribia mtoto masomo hayo, ni amsomeshe, amhudumie mpaka ajifungue na amurudishe shule, asome na mtoto wake amlee.

Na upande wa ardhi asihusishe County Councils ahusishwe wazee.

Na upande wa vijana. Upande wa vijana, wa andikishwe kazi za Fisheries, vijana kutokewa area hini hini Pwani kwetu. Wawe ndiyo watakao kusimamia upande wa Idara wa Fisheries. Ijapo kuwa wengine hawaka kusoma, lakini wako wengi ambawo wame soma wame maliza, na wawe ni wawo, wahusishwe.

Na upande mwingine wa vikundi vya kina mama. Pia twataka ziwe serikali. Misaada yote ambawo inatoka inje, ipitie kwa kina mama. Ipitie kwa kina mama ihusishwe. Wakina mama ndiyo wenye tabu. Tuna beba mimba. Tuna lea watoto. Shida zote ziko kwa kina mama. Tunasikia ma Radio tu kutangaza misaada nini, nini, lakini hatufaidiki kwa chochote wakina mama. Tunasikia tu kwa ma Radio.

**Com. Maranga** – Maliza.

**Maimuna Omari Abdalla** – Nimemaliza

**Com. Maranga** – Asante Mama Maimuna Abdalla. Tuweke sahihi kitabu chetu please. Tuweke sahihi kwanza kabla huja toka. Mwingine ni Ebrahim Hirbai. O.K. una dakika chache kabisa.

**Ebrahim Hirbai** – Asalamaleikum. Kwa jina ni Ebrahim Hirbai kutoka Ozi, Sub-Location, Kipini Location. Utangulizi. Na

anza na utangulizi. Wimbo wa Taifa kama kawaida.

Ardhi ipewe wazaliwa wa Tana River kuliko hii mutu kama Waithera, Musyoka kutoka Nairobi huko awe ako na Tittle Deed Tana River na mzaliwa wa Tana River iwe hana.

Tunakuja upande wa Elimu. Elimu imekua ngumu kwa sababu tumekuta kuanzia shule za Msingi hadi za Upili, karo ime panda sana. Tunaomba ikiwezekana Katiba hii mpya mambo ya Karo iayarudi kama 1970's vile ilikua.

Tunakuja kwa employment, uajiri. Kila mutu aajiriwe kwa Wilaya yake. Si mutu kutoka Taita Taveta aje aajiriwe Tana River. Katika employment, hiyo hiyo, tunakuja administration. Chiefs, tunaomba ikiwezekana katika Katiba mpya hii, iwe upande wa Chief, si serikali wenye ku interview ama kuhoji maswali, bali iwe raia wenyewe wapewe hii jukumu wawe na kura zile za mlolongo kuliko watu waende wawekwe kwa interviews na ule pengine mutu kama huyo ni mbovu, na aletwe kuja kuhudumia raia.

Katika Radio, tunasikiza mambo kama ya kunajisiwa. Mara nyingi sana inazungungumuzwa. Tunaomba katika Katiba mpya hii, wanawake ziwe zile nguo zawo za kuvaa, ziwe nguo zenye heshima na wakati huyu mama atashikwa awe na nguo ambawo ina heshima, ajaribu apelekwe Mahakamani, na ajibu maswali. Kwa sababu kuna huu mutindo mpya ume toka, mutu anavaa nguo ina andikwa , "Things are here", mambo yako huku, unaona? Kwa hivyo nguo kama hizo style, skin tight, unakuta mutu amevaa nguo, underpants, chupi iko inje. Kwa hivyo tunaomba pia, mambo kama hayo ndiyo ambawo yana leta hiyo matatizo ya watu wana shikwa, ku repiwa ama, unaona? Kwa hivyo asanteni sana.

**Com. Maranga –** Asante. Mwingine ambaye naye mwita ni Salima Achilati. Salima Achilati? Ame enda. Salima, hamna. Haya Fatuma. Ndiyo huyo? O.K. Haya Salima.
Salim Achilati wakati ni wako.

**Salima Achilati** - Habari zenu?

**Com. Maranga –** Salama sawa sawa. Karibu.

**Salima Achilati –** Kwa jina naitwa Salima Achilati. Namimi zile record zetu …

**Com. Maranga –** Ongea na sauti. Kwa hivyo hauna maoni?

**Salima Achilati –** Ngama alisoma hapa. Maoni ni yale ambawo tumeandika pale. Niwasalimie alafu ni ende.

**Com. Maranga –** O.K. Nashukuru. Haya mwingine Fatuma Ali? Fatuma? Hayuko? Mwingine anayefuata Kiteme Mlatia. Kiteme? Hayuko? Haya mwingine…. O.K. Sawa sawa. Mwingine ambaye awe karibu kabisa ni Aluis Sheikh. Kiteme Mlatia anza na majina yako una dakika chache.

**Kiteme Mlatia –** Mimi ninaitwa Kiteme Mlatia, ninakaa hapa hapa Kipini, Shauri Moyo. Maoni yangu katika mageuzi ya Katiba…

**Com. Maranga –** Tafadhalini nyamazeni kidogo atoe maoni yake. Kimya kidogo. Endelea.

**Kiteme Mlatia –** Mimi ninaona kwa upande wa Rais wetu, awe chini ya sheria na asiwe mlevi, na awe amemujua Mungu. Na asiwe asha patikana na uuwizi mbeleni. Na awe yeye ni mpendwa wa watu. Na asipate uraisi kwa sababu mutu fulani wa kwao alikiwa mukubwa wakati fulani. Kwa hivyo huyo rais apate hicho cheo kupitia elimu yake na kupendwa na watu. Hiyo ndiyo maoni yangu ambawo ninataka yawe namna hiyo.

Na pia kwa upande wa ardhi, nataka iwe iko chini wa wazee wa mtaa. Na kama mutu amekaa mahali kwa miaka mitatu, ama zaidi, yeye anakula hapo anakunyua hapo, hata kama ni kwa kichua ya mwingine, na akae hapo, bora awe na amani na ni mwana Kenya.

Kwa upande wa mila, mimi maoni yangu naona mila isipingwe. Iwe ya nani, ya kabila gani, ya kabila gani, isi pingwe. Mila iendelee.

Pia, maoni yangu ninaona tohara kwa wasichana iendelee. Maanake, umalaya umekua mwingi sana kuliko zamani. Wakati kulikua tohara, azikua zime pingwa akukua na umalaya.

Lingine, kiongozi wa ngazi za juu serikalini aki iba, na adhibiwe na afutwe kazi.

**Com. Maranga –** Ume maliza?

**Kiteme Mlati –** Na pia ninaona ni vizuri Kenya iwe na elimu ya lazima. Kila mutu awe amesoma. Pia, ninaona ni vizuri mwalimu wa Nursery awe akilipua na serikali.

Pia maoni yangu, mutu akimuua mwenzake ama mwingine, na yeye pia awawe.

**Com. Maranga –** Maliza.

**Kiteme Mlati –** Mambo ya kuhongana kwetu Kenya isiweko. Wenye roho za kuhongana na kuhongwa waangaliwe sana mpaka wasionekane tena. Hiyo ni maoni yangu.

Na pia rais mume, na makamu yake mke.

Na kesi ya bibi na bwana isiende Kotini. Ifanywe na wazazi wa pande zote mbili. Asante.

**Com. Maranga –** Asante sana kwa maoni yako. Weka sahihi hapo na utupatie memorandum yako. Anaye fuata Bwana Aluis Sheikh. Wapi Sheikh? Sheikh? Hayuko. Izack Kakuti? Izack Kakuti? Haya.

**Izack Kakuti –** Mimi kwa majina naitwa Izack Kakuti. Nachangia Katiba na mambo matatu.

Jambo la kwanza ni kuhusu hospitali. Wakati Kenya ilipata uhuru tulikua wananchi wakipata matibabu bure na wakatu huu umekuwa mwananchi halisi akipata maradhi, yule wa hali wa chini anaweza kufa nyumbani pasipo kuwa na pesa ya kuenda kulipa hospitalini.

Pili, wanyama wa pori. Kweli haya mambo yamekwisha zungumuzwa na watu wengi lakini serikali imekua wanyama wa pori wakubwa kuliko mwanaadamu. Kwa sababu mwanaadamu ulima na wanyama wakati walipo kuja kumharibia Shamba Lake, anapo peleka ripoti katika kituo cha polisi, ana ambiwa hakuna malipo. Mwananchi anabaki aki tangatanga hana chakula, wanyama wamekua ndiyo wenye nafasi ya kuweza kuchangilia zaidi kuliko mwanaadamu wakati wana nyanyaswa na wanyama.

Tatu. Ni mambo ya ardhi. Tangu Kenya inapo jinyakulia uhuru, tuliambiwa kwamba mashamba haki itakua katika wananchi. Wakati huu, mashamba imeshakua, ni wale matajiri, unaweza kuona sehemu ya ekari karibu elufu nne inachukuliwa na mtu moja. Mwananchi yule, yule alikuwa akinyanyaswa akipigania uhuru, ime ua kwake, hana mahali pa kukaa, anakaa kwenye mapango ama kwenye milima. Hayo ndiyo ninaomba Katiba kama inawezekana wajiribu kuangalia. Asanteni.

**Com. Maranga –** Asante. Basi asante kwa maoni yako. Utuweke sahihi kitabu chetu rasmi na asante kwa maoni yako. Mwingine anaye fuata ni John Jalua. Si ali ongea? Ama … John. John Jalua? Hayuko. O.K. sawa.

Speaker – John Jalua ako District Health atakuja.

**Com. Maranga –** Sawa.

**John Jalua –** Asante. Majina yangu naitwa John Jalua. Na nilikua nikitaka kuichangia kwa upande wa Pension Department.

Pension Department kwamba iondolewe na badala yake, wale waajiriwa, wawe wakisimamiwa malipo yawo na ile Wizara yao, ambawo alikua akifanyia kazi.

Na wako wazee wengi ambawo kuamba hawajimudu katika maisha yawo wakati huu. Na mimi napendekeza kwamba wazee wetu wakifikia umri wa miaka sitini, na kuendelea wapewe pension.

Mbunge au Councillor, akitaka kugombea kiti, asiwe ambaye kwamba, ambaye amehusika na jambo la kashfa, pengine ya uwizi ama ya Kotini, ama ya uchochezi wa vita. Akipatikana na mambo kama hayo, asiruhusiwe kugombea kiti hicho.

Kwa upande wa Wilaya, ningependekeza kwamba DC asiwe muhusika, kuwa mwenyekiti wa maendeleo Wilayani. Awe ni mutu wa utawala, na badala yake kuwe na mwenyeji ambayo kwamba atasimamia na ambaye atachaguliwa na wananchi wenyewe, na asi hudumu labda zaidi ya miaka mitatu hivi, ikiwako anachaguliwa mwingine.

Kuna mutindo siku hizi, watoto wakimaliza shule, waki itwa kwa ma interview, unasikia peleka form yako ama baruwa yako ya maombi na shilingi mia tano ndiyo ukubaliwe. Mimi nafikiri mtindo huwo ingeondolewa kwa sababu wale watoto ni wenye kutafuta, na misigo kama hiyo ni shida.

Na la mwisho ni kwamba, hawa KPR, walipwe mishahara na wawe na elimu ambawo kwamba isiwe duni ya kilasi cha saba. Na wawe na umuri mzuri ambawo kwamba, wanaweza kusimamia vijiji vyawo vizuri. Asanteni.

**Com. Maranga –** Asante Bw. John. Pengine utuwekee sahihi kitabu chetu rasmi. Mwingine anaye fuata ni Daniel Arubo. Daniel. Daniel Arubo? Daniel? O.K. sawa. Wewe ndiyo yeye? Haya maoni yako.

**Daniel Arubo –** Nawasalimu kwa jina la Yesu. Kwa majina naitwa Daniel, Arubo. Nimukaaji ya Tana River, ni askari wa Utawala.

Maoni yangu jambo la kwanza ni kuhusu Kilimo. Kama unavyojua kilimo ndiyo uti wa mgongo katika maisha ya mwafrika. Lakini hali ya kilimo umerudi chini kwa sababu serikali inatoa facilities, natoa pesa za kusaidia hali ya wananchi katika hali ya kuinua kilimo. Lakini utakuta kwamba, wananchi ni masikini kama hivi sasa, nimusimu ya mvua watu hawana mbegu, hawana dawa na hawana elimu ifaayo kwa kuwainua katika hali yawo ya kilimo. Na ma officer wa serikali wako. Kwa hivyo ninapendekeza Katiba kama vile ilivyo panga, kama vile kuna huduma hawo basi watekeleze majukumu yawo ili kila mtu afaidike kulingana na kile anacho kifanya.

Jambo la pili, nitazungumuza kuhusu ndoa. Mwanaadamu amepewa huru wa kuwowa. Lakini heshima hii imepungua kwa sababu ndoa zime kuwa maisha ya kiholela holela. Mutu leo anawowa hapa, kesho ana divorce, anaowa hapa, kesho ana

divorce. Lakini anapo owa anazaa mtoto. Mtoto huyu atakua mali ya nani? Kwa hivyo taifa Mungu anadai haki za watu sasa. Kama munavyo masikini vile unavyo ingia ulimwenguni, ni kwa sababu watu wameacha hadhi za wanaadamu. Watu wameacha kuhadimika kimila, kidesturi. Hata katika misinga za dini zetu. Kwa hivyo nina himiza sana ikiwezekana, kila anaowa aimiliki. Hata ukitaka owa kumi, lakini amiliki. Sio kuowa na kuwacha. Hapana. Leo nakataa. Maoni yangu.

**Com. Maranga** – Asante.

**Daniel Arubo** – Jambo la tatu, nitaongea kuhusu elimu. Kama wengine wanavyo sema kuhusu elimu yetu, sehemu zetu za rural areas, watu ni wamasikini sana. Tunaomba ile mipango ya Development Committees wanapo panga mambo ya bursary funds, tafadhali serikali nayo iweke fund fulani ya kusaidia watoto hawo ili kuamba awa boost katika hali ya ki elimu.

Ya la nne nitaongea kuhusu askari. Kama muna niona hapa ni askari. Mimi ni mtaalam. Mukubali, musikubali, ni mtaalam kupambana na majangili. Niwe na bunduki, nisiwe na bunduki. Lakini mshahara yangu ni duni. Na kuna wengine hapa kwa sababu ya elimu walionayo, wanalipwa mshahara mnono, kwa nini? Basi na huwo serikali, kwani kuna tofauti gani? Na mimi nimejitolea mihamba hadi kufa kwa sababu ya uma. Kwa nini nisilipwi mpasavyo? Kwa nini na kaa nyumba duni? Kwa hivyo mutu anapo taja askari hapa, jihoji sana wewe unataka askari. Nimejitolea mihamba hadi kufa, kwa sababu yako wewe. Na wewe leo unaniambia mimi nakunyanyasa. Ninacho sema ni kwamba Katiba yetu, iangalia huduma isi angalie mambo ya elimu, kwa sababu kama ni elimu, kuna sehemu fulani ambazo mutu atafanya. Lakini watu hawajitolee, wanataka mishahara peke yake. Basi mimi si semi mshahara, ni askari na niko tayari kufa kwa sababu ya Kenya. Nitaongea juu ya District Focus.

**Com. Maranga** – Basi, ya mwisho kabisa.

**Daniel Arubo** – Dakika zangu bado bwana. District Focus ilikuwa ni mpango wa serikali katika mashina, mpango huu haukufaidisha. Sijui sehemu zingine lakini sisi haikutufaidisha. Afadhali wakati ule ambapo serikali inafanya mambo Nairobi, inafanya miradi hapa. Tumefaidika. Leo miradi hiyo imekufa kwa sababu ya machache wetu ambawo wali grab, naongea sana?

**Com. Maranga** – Asante

**Daniel Arubo** – La mwisho kabisa, inflation.

**Com. Maranga** – Ongea tu kwa hiyo ndiyo…

**Daniel Kubo** - Inflation imekumba maisha ya mwanaadam sasa, kwa sababu ya kutokua na mpangilio mzuri. Ninapendekeza kila mtu, ajihami kabisa, kabisa, ajitowe mihami katika maisha, ili jamii alio nayo aimiliki, ili Mungu naye apato utukufu,

mwanaadamu naye apate utukufu, serikali isisumbuke kwa ajili ya jamii ambazo za kiholela holela. Mungu awabariki sana. Karibuni.

**Com. Maranga –** Asante sana.

**Com. Maranga –** Asante sana Bw. Daniel Arubo. Tuwekee sahihi kitabu chetu rasmi. Hiyo maoni yako niya muhimu, na asante sana. Mwingine ni George Amuma. George? George Amuma? Ninataka kusema kuwa mutu yoyote anahaki kutoa maoni mbele ya Tume ya kurekebisha Katiba, uwe mufanyi kazi ya serikali, ama sio mufanyikazi wa serikali, kwa hivyo huyu Daniel ametoa maneno mazuri sana, nafikiri. Kwa hivyo asante sana Bw. Kubo, maoni yako itatusaidia sana kushugulikia Jeshi la Police. Asante sana.

**Daniel Kubo –** Thank you Sir.

**Com. Maranga –** George Amuma?

**George Amuma –** Yes. Kwajina naitwa George Amuma.

**Com. Maranga –** Amumo au Amuma?

**George Amuma –** Amuma. Amuma. Nimfanyikazi wa Agriculture Office, na mimi ni nakaa hapa Kipini.

**Com. Maranga –** Haya ufanye maoni yako kwa haraka sana.

**George Amuma –** Kwa ufupi maoni yangu ni matano, na ni kwa ufupi, si historia. Jambo la kwanza wenzangu wametaja ni kuhusu ugaidi. Ugaidi imekua ni kitu cha kawaida katika Kenya kwa jumla. Maana ake tumekaa kama ambawo kwamba hatuna dini. Iko dini mbili Mungu ametuletea tufuate lakini hatuna. Kwa hivyo sasa katika ugaidi, kumekua kitu cha kwanza, ambapo kwamba wale magaidi, hawawezi kuchukuliwa hatua kikamilifu wakafanyua kama mkoloni alivyo fanya, kuwamaliza wale magaidi kabisa, na kila moja akaona kwamba huyu mutu amemalizwa, kwa ajili ya kwamba yule mgaidi akirudi kesho, atamfundishwa yule mwingine. Gaidi akiuwa mtu, atakuja, ukimuacha tena, atakuja kumfundisha mtu mwingine hata mimi mwenyewe, sijui. Hilo naomba ikiwezekana, Katiba iangalie. Ugaidi. Umekua kawaida. Hata kama unapita bara barani wewe unakwenda kwa shambani kwako, unaenda mjini kwako, jamaa anakuotea njiani anakumaliza. Uko town, unatembea, humu watoto wako wamejua umekwenda kazini, unaona unamalizwa. Ugaidi umekuwa jambo la kawaida Kenya. Liangaliwe sana.

Ya pili ni mazingira ya inchi. Mazingira ya inchi nafikiri watu wanapo tembeya kama hapa, sidhani kama hapa kutakuwa na

manyasi tena.  Haya manyasi yata kauka kabisa.  Nafikiri kila moja atajionea hapa.  Ijapokuwa hapa watu hawatembee, hapo wana tembeya, unakuta hapo pana manyasi, na hapa hapana manyasi.  Kwa ajili ya nini, kwa jili ya kwamba, tuna semea kulingana na yani upande wa ukulima, ukulima na mifugo, wafugaji.  Wafugaji ni watu wetu, nasoto tuwamoja, naweza kujitolea nikawa mfugaji, lakini katika ufugaji wangu, kumepita kiasi cha kwamba nitakua na mifugo mingi, ambayo kwamba nikimwaga hapa, hata mimi nikija ni kesho, mwingine akija kulima, hawezi kupata kitu.  Nafikiri hapa ukiangalia sehemu hii ya Kipini, hamwezi kuona wafugaji ya mifugo mingi, na ndiyo munaona hii miti hii.  Kwa ajili ya mazingira yana chungwa, lakini ukienda sehemu zingine, kama sehemu za mtoni zile, unakuta hata shamba ya mutu imekauka, wee enda ukaingize jembe saa hii kume nyesha mvua, haikuwezi kukua kitu.  Hakuna kitu kitakua.  Kwa ajili ya nini?  Mifugo mingi, linakausha kabisa.  Hilo jambo tungeomba kabisa Katiba, muangalie katika hali ya wakulima na wafugaji, kwamba sheria yao itawekwa kinamnagani?

Jambo lingine la tatu, ni msaada ya washirika.  Hawa washirika wanao, mashirika tuseme, yanao ingia humu kwetu. Tunasikia mashirika mengi yana kuja yakunifaisha wale ambawo kwamba ni duni, lakini tunaona kwamba yale mashirika wenye pesa, ambawo kwamba wangenufaisha wananchi, wanabaki Nairobi, ambapo kwamba sasa kama sisi, kama wananchi namna hii, hawajui.  Tunaangalia, mukiangalia shirika moja ambalo kwanza mutaona mfano, iangalieni GTZ, hivi sasa ana mfajo wa kutosha, kuonyesha kwamba katika sehemu hii, GTZ amefanya kazi ya kutosha.  Nafikiri mutaone ufano wake, jinsi alivyo fanya kazi mashambani na mifereji, jinsi inavyo wekwa.  Tungetaka mashirika kama yale yakuwaonyesha wananchi nawo wakanufaika.  Nafikiri jambo kama hilo mwangalie ya kwamba, katika hawo ni shirika gani ambalo kwamba italeta maendeleo na ku wale wananchi waweweza kunufaika zaidi.

Jambo la nne ni mishahara ya watu duni, kama sisi.  Mishahara tunasikia kwamba Kenya haina pesa.  Imezoroteka, lakini baada ya kutangaza wajumbe wamejipangia mishahara ya juu, wana karibu million moja.  Jee hizi pesa, wanazichukuwa wapi?  Mimi sina mengi kutokana na hiyo number four.  Wanazichukuwa wapi, hizi pesa wanazichukuwa wapi?  Na wamesema hakuna pesa.  Na hilo jambo lijaribu kuangaliwa, nasi tunufaike kama wawo.

Jambo la tano, ni muda.  Sasa sisi tunachukuwa miaka mingi, watumishi, kufanya miaka mingi kwa kazi, mpaka tukashike gongo, ndiyo twende retire.  Kwanini huyu mtu, ambaye kwamba, je anangojea kwamba naye aonje matunda ya Kenya. Mbona hawezi kupata nafasi, apate hiyo nafasi?  Kwa nini haipungunzwe.  Nikisema pengine moja wapo, lakini ningeomba ikiwezekana jambo hili liangaliwe sana kwamba kuna vijana wetu, kuna wajukuu wetu, nawo wana angalia hapo, nawo wapate yale matunda.  Muda, ule muda wa retire, uchunguzwe sana, ili ya kwamba hawa wa nyuma nawo wapate.

**Com. Maranga –** Haya, malizia mzee wangu.

**George Amuma –** Nafikiri hapo nimefikia mwisho.  Sina zaidi.

**Com. Maranga –** Nashukuru.  Weka sahihi kitabu chetu rasmi na ninashukuru kwa maoni yako.  Mwingine ni Ali Muhamed.

Ali Muhamed. Haya. Nafasi ni yako.

**Ali Muhamed –** Habari zenu? Mimi ni Ali Muhamed, mzee kutoka Kipini. Maoni yangu nikama haya nayo fuata ati. Kuhusu habari ya ardhi, ningependelea Council na baraza la wazee mahali panao fika, ipewe uwezo na Serikali kusuluhisha matatizo yao ya ki ardhi na pia nakugawanya, na kiutawala. Wale wazee walioko pale, wawe na uwezo pamoja na Council kumupa mutu na kupatiwa uwezo mpaka kupewa kitambulisho kamili cha ardhi.

Jambo la pili, ilikuwa kuhusu uvuvi. Uvuvi huku kwetu Pwani, ni uvuvi ambawo ni wa bahari,
pia maziwa na mito vile vile, na vile ikiwa ni bahari ni sehemu kubwa na uwanja mkubwa wa huu uvuvi, na ikiwa ni hivo pia na mazawo na mambo yake yote ya kivuvi lazima makubwa. Lakini mpaka wa leo, sisi tumemaliza nusu karne ya uhuru, hatujawa hata kiwanda kimoja sisi, cha uvuvi hapa. Hii machi ya vifaa au ya mazao ya kutoma baharini. Leo, hivi juzi tu kume fumuliwa kiwanda kumeanzishwa huku maaridi katika Lake Victoria chenye cha million mia nne. Leo huku Pwani hatuna hata tawa ya million moja na vifaa vingi vinagawanywa huku, na nimesha shuhudia kamati kadhaa zime pangwa Wilayani kwetu Tana River kutowa mikopo kwa wavuvi ambawo wako kwenye maziwa, na mto na baharini, na wakati mimi nikiwa mmoja katika hio member, tuliambiwa pesa tiyari ziko office ya DC. Sisi ni kushuhulika kuteguwa Kamati na mara moja pesa zitoke. Kamati hizo zote silipita muda zika fifia na hakuna habari za zaidi zilipatikana.
Huko juu bado kunatolewa ma Boat, ma Nyavu, watu wananufaika, wavuvi wanabadilika hali zao, na hali kwetu Pwani tunaona mvuvi bado anasinyalo, kila kuchapwa na kwenda chini, mazawo yana kwenda chini, lakini wale wenye nguvu sana, mazao yao yana panda juu. Nikuonesha mazawo yako lakini wanasinywa kabisa wale wavuvi wa chini, wasiweze kuinuka. Na mambo haya bilashaka kwa kwenye sheria inajulikana, kwa hio sheria itengenezwe. Ule uwezekano kupate kikopo sehemu zote za Kenya zinazohusika wapate kikawadia na ambawo hakuna basi zisiweko. Lakini tukisikia Pwani hakuna kitu, lakini Lake Victoria viwanda vinatengenezwa samaki, hii inatumiza roho.

Jambo la tatu ni katika habari ya uhamisho (Immigration), kugura baada ya nchi na nchi. Vitambulisho za kuweza kuguria, yani Passports, uku kwetu umekuwa kawaida, tena tunambiwa Pwani ni tabu kupata kwa sababu wageni ni wengi. Lakini tunamajeshi mpakani sisi, wanalinda mipaka, na wanajua nani anaingia, nani anatoka. Bahari tuna Navy, wanajua nani anapita, nani anarudi, nani anakwenda. Leo, kwa nini wasisumbwe kule mipaka na bahari, wakaaja kumsumbuwa mtu kijijini asipewe Passport? Anaasilia, anaasilia nini? Kule kando, kando wanalinda nini ikiwa ni hivyo? Kwa hiyo iwekwe sheria hivi vitambulisho vitoke kwa urahisi kwa ule mwananchi, mwenye kufuatia masomo apate, mwenye kufuatia kazi aende, mwenye kwenda hija aende, kila jambo liwa rahisi kinamna hiyo, vitambulisho vya usafiri vitoke kwa urahisi Mkowani Pwani.

Jambo la tatu, mwanzo wa Katiba, kutunga Katiba, Katiba yetu hii ambawo iko, tuna ipua kwenye jungu, haina jina la Mungu, mwanzo wala mwisho alakati. Kwa hio mwanzo wa Katiba yetu tunataka tuliweke jina La Mungu, Kati. Mungu, nikisema Mungu ule mwenye dini atajua, mwenye mzimo a tena atajua yeye huko.

Muundo wa serikali. Serikali tunataka tuunde ya Majimbo bwana. Kwa sababu serikali, tukonawo PC, lakini baado hata ukiwa Mombasa, uona uko mbali sana na ule mtu wa chini. Kwa hiyo tujaribu kujiongeza karibu, tukiwa na Majimbo, huenda tukawa karibu nawo na tukaweza kupata mwene mufunuo mwingine wa nchi.pamoja na nchi nzima na jimbo letu.

**Com. Maranga** – Haya malizia Ali.

**Ali Muhamed** – Haya, uwezo wa Bunge, namalizia hapa kidogo. Uwezo wa Bunge utaka ufikiriwe. Upunguzi ijapo kuwa tume muchagua mbunge, lakini kuwa na madadi zingine maalum mpaka arudi kwa wananchi, kwa sababu nitawapa mfano moja hapa, kuna waalimu wanaya liya hapa, wanataka mshahara waongezewe, miaka mitano, nasikia saa hizi inatiwa kesho zina ambiwa zime futika. Lakini, Bunge ilipo pitisha mshahara uwe mkubwa, leo impitishwa, kesho pokea cheque ya mshahara wake. Kwa hiyo hapo ipunguzwe.

Uwezo wa serikali. Huwe na uwezo wa serikali mimi nikiwa nina madaraka makubwa siku hizi, uwendelea kwangu mpaka nika jenge nchi nyingine huko ngambo zunguni, kwambia ndiyo kuna usalama wa pesa na rasili mali, nikaweke ma cheque na nini. Kwa hiyo, wananchi, au serikali ikigunduwa mambo kama hayo, umeteka nchi na inje una uhalifu, iwe na uwezo za kuchukuwa zile zirudi nchini zitumike kwa wananchi.

**Com. Maranga** – Asante Ali Muhamed. Malizia sasa.

**Ali Muhamed** – Haya namalizia hapa. Ebu kuwa kumebaki kuhusu Mahakama. Mahakama iwe na uwezo kwa wale wanaofanya ufisadi kwetu, TKK imekua familia maanake ni kitu cha kawaida. Hata mutu anawo uwezo mpaka kusema, itafanyika je kazi bila TKK? Kwa hiyo Mahakama iwe na uwezo mfanyikazi wowote isichukuwe muda mrefu, akingunduliwa na kalamu ipite hapo hapo. Kwa sababu atoikuwa maanake ajua mimi nitafanya corruption, kupigwa transfer kitu cha zaidi, lakini akijuwe corruption ikilijulikana, masaa matatu, aenda nyumbani akishike brake.

**Com. Maranga** – Asante Bw. Ali Muhamed. Tuweke sahihi kitabu chetu rasmi. Asante kwa maoni yako. Mwingine tunayemuita ni Thomas Paul Guiyo. Thomas? Haya. Wakati ni wako.

**Thomas Paulo Guiyo** – Hapo mwanzo nilikuwa membe wa Majimbo, kwa hiyo jambo la kwanza nataka Kenya iwe chini ya majimbo. Kila mtu kwao.

Kitu cha pili, ni kwamba kwa sasa uwezo wa County Council iko chini ya Clerk of County Council. Kwa upande wangu mimi naona ni makosa maana huyo aja andikwa na County Council, kwa hiyo Chairman awe na uwezo kuliko huyu Clerk katika County Council maanke ni mtumishi wake. Na pia, na wale Councillors nawo wawe na uwezo kuliko huyu ambaye ni Karani wao.

Kitu cha pili Bw., ile kiongozi wa Kamati hii, maoni yangu ni kwamba kama Councillor ama mjumbe ameenda Bungeni, ama aeendea kwa County Council, ikiwa wafanyi kazi wananchi wawe na uwezo, mtu huyo wamfute, watie mwingine, si kwamba yeye ni Councillor, ama ni MP, basi aringe huko na kwenda wapi, na huko atufai. Kwa hiyo, wananchi wawe na uwezo wakumtoa mtu huyo, na kutia mwingine, ikiwa Kamati itakubali ama hii serikali itakubali, hii katika Katiba yetu mpya iwe namna hiyo. Asanteni.

**Com. Maranga –** Asante Mzee Guiyo, asante kabisa, umetoa maoni ya muhimu, na utuweke kitabu chetu rasmi sahihi. Mwingine tunamuita ni Amina Banda. Amina Banda? Amina? O.K. Haya mama karibu.

**Amina Banda –** Mimi naitwa Amina Banda. Kwa kuongeza maneno ya yule mama. Tuna lalamika habari ya watoto. Hawa watoto wa siku hizi, hakuna wavulana, hakuna wasichana, hawana heshima iliotosha, maanake, katika masomo, hakuna kuangalia masomo peke yake, wanaangalia masomo, na mambo mingine. Hasa yale masomo yawo hayako sawa sawa, sijui tena ka huku town, kama huko kwetu risafu risafu, masomo haendi sawa sawa, na watu wanapata shida, na ma bwana siku hizi, mwanamuke asimame na watoto, kitabu, kalamu, waona, kila kitu ni mwanamuke. Na watoto wawo wenyewe, baada ya kufikiria, wanasumbuana, kwa habari ya furaha, furaha na habari ya starehe, starehe. Kwa hivyo hiyo Katiba, ambawo itapangwa sasa, mutaanza upangilio kwa watoto. Watoto wawe sawa sawa, wakujataidi, na heshima nzuri, na kujua maisha yawo. Maana starehe mingi inapoteza maisha, haina maana.

La pili, tuna huzuni, wakina mama siku hizi, na hawa akina baba. Kina baba hawana huduma za kisawa mazumbani kwa akina mama. Ni hawo serikali mupange, upangilio ya sawa sawa iwe haya maisha kila hakuna huduma, ile serikali wana mipango maalumu, wakuwakamilishia huyu baba na mama wawe sawa. Maana mume atakuwowa mkiwa msichana, yeye ni mvulana. Mukiendelea siku mbili, tatu, mukiwa na watoto wa nne wa tano, labda ataona ile paketi moja ya maziwa awezi kunyua tea sawa sawa, ameanza kuangalia kwingine iwe kule ni pekee yake, apate kunyua chai nzuri ya maziwa, apate kila kitu. Ukiamwa, kule nyumbani uki amuka, kama huko rizavu, mwanamuke akiamuka, aangalie mambo ya kula, aende kwa vibaruwa, sijui nini, mwanamuke ana kibaruwa, na wale wazee wetu walikua hawana elimu, hawana kitu chochote, lakini mama anavaa nguo, na mtoto yuko nyumbani na adabu zake, umwoni kwenda nyumba ya mutu, akaote kula, na wala hakuna kila neno.

Sasa wewe ukiuliza bwana anasema ati wanawake wanamatamanio mengi. Si bwana kwani tuna matamanio? Kwa nini mwaona yeye ajifanyia yale matamanio yake ikiwa ni begi nzuri, ikiwa ni kiatu kizuri, kila kitu? Lakini sasa tugawanyane, bibi, uniform ya mtoto, bei inashinda bwana kumnunulia. Bibi aende kwenye vibarua amnunulie uniform mtoto, kila haku nunua, mtoto anasoma hivyo, hivyo, na nguo ambaye asha cheza chini ya mti. Kwa hivyo serikali hii Katiba ya leo ipange maisha sawa, sawa wakina baba na akina mama, tuwe na msingi maalumu wa kuishi majumbani kuangalia watoto wetu. Ni haya.

**Com. Maranga –** O.K. Asante mama. Mwingine ambaye namwita ni Samuel Kinuthia. Samuel?

**Samuel Kinuthia –** Majina ni Samuel Kinuthia

**Com. Maranga –** Kwa ufupi kabisa mzee wangu.

**Samuel Kinuthia –** Kwa upi? Kwa jina Naitwa Samuel Kinuthia, mkaaji wa Kipini katika sehemu ya Shauri Moyo. Kuna mambo kadhaa ningetaka niyachangie, nayo ya kwanza ni Maji. Katika sehemu hii au sehemu zingine zinaonekana, maji mahali wananchi wako, hakuna maji ya kutosha. Au pengine hakuna maji watu wanaenda sehemu mbali kutafuta maji na mtu hawezi akakaa bila kuwa na maji. Maji yanatakikana mahali popote, sheria itayarishwe yakuonyesha, mahali kuna mtu, lazima kuwe na maji ya kumtoshelesha

Mawasiliano. Mawasiliano ni muhimu sana, na kama hatuna simum hatuna mabarabara, kama tuseme, kutoka Witu mpaka hapa, barabara ni mbovu sana. Kwa hivyo sasa, kila mahali na kunaonekana kuna watu lazima kuwe na mawasiliano inawo inawostahili, kwa sababu kuna mengi ambawo wanatakikana kujilikana mahali lakini, mawasiliano ikawa ni mbaya. Mawasiliano sheria itengenezwe yakuonyesha kila mahali kuna mwananchi, mawasiliano yawe ni mazuri.

Wakulima. Wakulima kutaarishwe sheria ya kuwalinda ili wakiweze kulima chochote wameshalima wasiwe wananyanyaswa, waangaliwe sana, kama ni kitu wanataka kuuza, waonyeshwe mahali pa kuuza, wameonyeshwe mahali pakulima, ikisha kuwa tayari, kuna wengine wanakuja ku wanyanyasha, kama ni kuuza, waonyeshwe hata kama ni nga'mbo kwenda kuuza kile amesha lima. Kwa hivyo, kutayarishwe sheria ya kuonyesha. Mukulima asinyanyashwe kutoka muazo mpka mahali mahitaji itakomalizikia.

Elimu. Elimu imekua ni kidogo sana. Watoto, kila mahali tuseme kama area hii, ninge tembea, tembea naona watoto wengi hawako katika shule. Na hii, ni kwa sababu, karo, mashule hayamo ya kutosha. Tena watu wazima hawana, kuna wengi ambawo nimewanauliza, wakaniambia, hata kusoma hawakusoma, hii inatakikana, sheria iundwe yakuonyesha kila moja, awe anatembelewa na elimu, amesha pata yakutosha kawaida, aweze hata kuandika hata jina lake, au kijitilia sahihi mahali popote inayo takikana.

Mwananchi wa kawaida asaidiwe. Mwananchi ya kawaida ndiyo anaonekana yeye ako chini sana, hata awezi kwa mwaka kujiwekea hata shilingi mia tano au hata shillingi elefu moja awezi akajiwekea. Ni kwa sababu kila wakati, anaonekana kama ni mtumwa kwa wale ambawo ni wakubwa. Mahali popote anapo enda, anapatiwa kama ni kibarua, anapatiwa kitu kidogo ili aweze, kesho yake kurudi, kwa hivyo anaonekana ananyanyaswa na njia zote, mukulima au mwananchi wa kawaida, apate cha kumsaidia, kutoka kwa serikali na sheria iundwe ili watu wowote, katika Kenya wawe ni sawa na wanapata mapato ya kutosha. Ni hayo tu.

**Com. Maranga –** Asante Mzee Kinuthia na tuweke sahihi kitabu chetu rasmi. Mwingine ambawo mimi namwita ni Maimuna

Omar. Maimuna Omar? Amesha ongea. Na Hussein Abdalla Ali ameongea. Haya kwa ufupi kabisa.

**Hussein Abdalla** – Mimi jina langu ni Hussein Abdalla Ali. Cheo ni Chama Cha Kipini Fisherman Association Marine Conservation. Mapendekezo ni ya local Fisherman. Bahari iwe chini yetu, sisi tulioko kwenye rasili mali hiyo. Kazi zinazo husu bahari iwe na usumamizi wetu wenyewe, ilioko kwenye rasili mali hio. Mfano, nilienda na officer, uhusika wa Fisheries kufanya awareness campaign ya kuwatambuwe hawa local fishermen umuhimu wa leseni. Na nikaingia naye kwenye mdawu, nikamuliza, unajua kuogeleya hili dawo linapo pinduka? Akanambia hajui. Na tunampango wa kufungua centre ya research. Sasa ikiwa tumetembelewa na wale wageni kutoka sehemu mbali, wanataka kwenda kufanya hio research, na huyu officer uhusika ikiwa yeye hajui kuogelea, tukienda kwa hiyo research, anaweza kupeleka hawa wageni hapo kuwaonyesha kwamba sisi tunaangalia kama coral ama malisho ya Kasa, mahali Kasa anapo lala, mapendekezo yetu ni kwamba mambo ya fisheries tuyasimamie wenyewe. Tunaoweza kufanya hizo shuhuli. Sina mengi zaidi ya hayo.

**Com. Maranga** – Asante Bw. Hussein Abdalla Ali na tunakuomba utuwekee sahihi kitabu chetu rasmi na asante kwa maoni yako. Sasa ambaye ninamuita sasa ni Danson Mungata ambaye ni….., No, ni Mngata, ni Mngatana ambaye ni Wakili, ebu tusikie maoni yake, una dakika tano ndugu yangu. You give us a summary of the main issues.

**Danson Mngatana**- I will and I will not talk for long. I will not talk for long. Wananchi ile Constititution ambaco tunazungumuzia ni hichi kitabu hichi, nacho, niko na mapendekezo fulani. Jina naitwa Mngatana. Mngatana. Danson Buya Mngatana.

Jambo la kwanza, ni kwamba, Constitution yetu, makosa makubwa yali fanyika katika kipengele cha kwanza. Kipengele cha kwanza, yani Pre-amble. Kibwagizo hapa katika Kenya Constititution hakuna. Section One ya Constitition yetu inasema Kenya is a Sovereign Republic yani, nchi yetu ni inchi ilio huru, lakini haielezei uhuru huu tutawu enjoy au tutausimamia namna gani? Sisi watu wa Tana River, tumekosa kutambulika katika Kenya hii, kwa sababu there is no direct recognition ya watu mpaka pande hii ya Tana River. Tunataka Pre-amble ya Kenya Constitution iseme kabisa ya kwamba ina recognize all the regional Provinces. Sisi tukiwa watu wa Tana River, na sisi tujulikane kwamba, katika Katiba, tuko na recognition, direct recognition, katika Pre-amble. Uki angalia Katiba ya inchi kama ya India, inasema India is a Sovereign State, comprising of various states, na katika hali ya kugawanya rasili mali, zile inchi zote, ambazo ni inchi za India, zinapata. Lakini ukiangalia leo, mutu wa Pwani, na mutu wa Tana River, tume nyimwa kwa sababu sheria hii haisemi kama sisi tuko. Ndiyo maana barabara ya Kabarnet inapigwa lami mpaka huko kwa ngombi wanaishi, lakini kutoka hapa Witu mpaka hapa, hatuna barabara.

**Com. Maranga** – Let me caution you Sir,

**Danson Mngatana** – Yes

**Com. Maranga –** Give views about how you feel, not political

**Danson Mngatana –** Sorry. Tunasema ya kwamba, haya nimakosa makubwa sana na ndiyo yame leta kuwekwa nyuma kwa mwanainchi wa Tana River. Ikiwa serikali ingekua inawekwa, by force, wanakuambiwa wakati munapanga budget, mwananchi wa Tana River naye lazima apate a certain section, tungekua hatuko katika mahali namna hiyo. Kwa hivyo katika hiyo Pre-amble, tunasema sana tukuwe recognized, mwananachi wa Tana River District.

Kitu ya pili, tunaomba new Constitution, ilete principle ya kwamba, na hiyo, hapo, hapo mwanzoni hapo, ya kwamba sehemu zile ambazo zilikuwa zimewachua nyuma, kama hii sehemu yetu, kwa muda wa miaka kama kumi na tano, ama ishirini, ipewe nafasi ya kuja juu na si tushike tuwe wakubwa kama hizi inchi zingine, majimbo kama Central Province na kwingine. Serikali kwa muda huu toka wakati ambawo tuta sign Constitution mpya, ifanye special programmes, ikiwa ni kwa hali ya education, tupewe nafasi zaidi, watu wa Tana River zaidi wapelekwe university. Ikiwa ni kwa hali ya kuandikwa ma kazi, watu, wa Tana River zaidi waandikwe ma kazikatika sehemu kubwa kubwa ili na sisi kwa miaka ishirini, tuwe tunapata discrimination fulani ambawo na sisi tutakuja juu, ama sivyo wananchi?

Wananachi – Ndiyo.

**Mngatana** - Tena ukiangalia Constitution hii imeweka siasa mbele kuliko mahitaji ya wananchi. Ukiangalia Section 1(a) ya hii Constitution, inasungumuza kwamba Kenya shall be a Multi-Party Democracy – Section 1(a). Haizungumuzii chakula chako wewe mwananchi. Haizungumuzii hali yako wewe ya kawaida, inakwenda kwa siasa. Ukiangalia Constitution ya inchi kama Iraq, Iraq, chakula chao kikubwa kinakuja kwa Fisheries, na Co-operative Society ya Fisheries, wameiweka mbele, mbele katika Constitution yao, na sisi tunaomba ya kwamba, mambo haya ya land, mambo ambayo yana muhusisha mwananchi wa kawaida, yawe in the fore-front katika Constitution yetu.

Inchi yetu haina political philosophy katika hii Katiba yetu. Ukiangalia, Kenya haija kuwa defined, haija semekana kwamba Kenya itakua inchi yaki communisti, itakua inchi ya ki Capitalisti, itakua inchi ya aina gani?

Constitution ambayo inakuja mpya, it must direct the state policy. Na hii state policy hii, ndiyo haya mambo munasema nyinyi wanainchi. State Policy, iseme kwamba, Kenya itakua African Social Democracy, na serikali ipewe compulsory katika Constitution, iambiwe lazima uhakikishe policy yote, serikali yoyote itasimamia mambo ya Social Democracy. Na hii Social Democrary, wananinchi tuna sema ndiyo hii ya kwamba tunataka compulsory free education kwa watoto wetu ambawo wanaenda shule. Sisi wote wanainchi wa Tana River hatuna pesa zaku wapeleka hawa watoto shule. Compulsory free education.

Ikiwa ni katika medical care, sipitali zetu hatuna pesa, tukiambiwa twende sipitali, tunaenda tuna andikiwa makaratasi

tunambiwa tukanunue, sisi hatuna pesa, wanainchi wa Tana River, kununua madawa katika ka hospitali ambawo ni private. Tunasema serikali yoyote, ambayo itachukuliwa, ikuwe ndiyo serikali itasimamia hii serikali ya Kenya, iwe iko na principle obligated under the Constitution ya African Social Democracy ili inchi yetu …

**Com. Maranga** – Malizia

**Danson Mngatana** – Sorry. Sorry, sita sema sana. Lakini, nataka kusema jambo moja, nikiwa namalizia. Ukiangalia wakatu huu, serikali ya Kenya na Constitution ya Kenya, imemupatia Rais, office ya Rais mamlaka makubwa sana. Na mamlaka haya ndiyo imekufanya wewe, na sisi wananchi wa Tana River kubaki nyuma. Wakati huu, serikali inasema kwa mfano, tukianza na hiyo office ya President, Section 4, Section 4 inasema Kenya itachagua Rais, haisemi kwamba atatoka wapi Rais huyo, atakua ni wa wapi, au atakuwa mutu wa namnagani? Inasema he will be the Commander-in-Chief, only. Sasa sisi tunaomba katika Katiba mpya, ya kwamba ikiwa serikali imesimamiwa na mtu kutoka Rift Valley, wakati huu, katika kisemo kitakacho kuja, iwe katika Katiba, iseme kabisa, ya kwamba serikali hii kama wewe ni mutu wa Rift Valley huta qualify kuwa president. Maanake hata sisi watu wa Pwani, na sisi tunakitaka hicho kiti, au sivyo?

**Wananachi** – Tunakitaka.

**Mngatana** - Ili tutoke hapo, twende kwa mutu wa Pwani, twende kwa mutu wa wapi? Na vyama viote ambawo vinapiganiya kuwa katika position ya President, wachague watu wao. Ikiwa the sitting President comes from Rift Valley, then hauna ruhusa ya wewe kama unatoka Rift Valley ku qualify, ili tupate nafasi kuwe na regional balances, maanake tukipata hayo maziwa nasisi (interjection)

**Com. Maranga** – We respect the Constitution

**Danson Mngatana** – Sorry, Mr. Chairman, sasa kwa hayo machache ambawo sijamaliza amenikata haba, lakini wacha tutasema zaidi.

**Com. Maranga** – Thank you

**Danson Mngatana** – I wish I could be given more time.

**Com. Maranga** – O.K. one more minute.

**Danson Mngatana** - One more minute. Asante sana. Na ukiangalia katika hii serikali yetu ya leo, Vice-President, Section 15 inasema, the Office of the President ita chagua Vice-President. Constitution mpya lazima ispecify huyu Vice-President atatoka

wapi? Na ni mtu wa wapi? Na iseme kabisa ya kwamba ikiwa President anatoka region flani, Vice-President atoke region ingine, pengine atoke Pwani, au Tana River yenyewe. Inshala, Mungu awabariki.

**Com. Maranga** – O.K. Thank you very------

**Danson Mngatana** – Na uki angalia on all other offices, saa hii, kwa mfano, serikali, hii Constitution inampa Rais nguvu yakupatia, hata kama ni ma Judge, inasema utachagua ma Judge, hai specify unatoka pande gani, unakwenda pande gani? Na kwa wakatu huu, Pwani nzima, hawa ma Judge ambawo wako wote, tuna Judge mmoja peke yake. Je hiyo ni kusema kuwa watu wa Pwani awafai kuwa ma Judge? Pia sisi tunataka hiyo pocho pocho. Kwa hivyo tunataka regional balancing katika everywhere, Public Service Commission, Permanent Secretaries, hatuna watu wa Pwanu, tuasema, Section 1ll ya Constitution inasema, utamweka Ambassador, Moi aka andika Ambassador, lakini aisemi, kuwa Ambassador itatoka wapi? Sisi watu wa Pwani tunawachwa, tunawachwa, tunawachwa, ukiona tabu tunapata hapa, ni kwa sababu kutoka juu, sheria hii imetuwacha sisi. Na sisi tunaomba ya kwamba, Katiba mpya iangalie kabisa mambo ya regional balancing. Niko na mengi ningependa kusema lakini kwa hesima ya Chairman, naomba tu. Asante sana bwana.

**Com. Maranga** – Haya weka sahihi Bwana Mngatana. Weka sahihi kitabu chetu rasmi na utupatie memorandam yako. Asante kwa maoni yako. Mwingine ambaye ninamwita ni Dickson Jilo Martin. Haya sawa. Utoe kwa ufupi bwana. Iko na watu wengine ambawo wanataka kuongoa.

**Dickson Jilo Martin** – Mimi ni mzaliwa wa Tana River, na naitwa Dickson Jilo Martin, na nilikuwa nataka kutoa mapendekezo yangu kuhusu Ufumo wa Serikali. Napendelea Ufumo wa Serikali ya majimbo Kwa sababu ufumo ulioko sasa umeshiwa kuleta maendeleo sawa katika maeneo yote. Pia napendekeza kuwa vitengo vya Serikali, yani Serikali, Bunge na Mahakama yagawanywe kwa nchi na kwa majimbo. Kila jimbo liwe na Bunge lake, kila jimbo liwe na Serikali yake, na kila jimbo liwe na Mahakama yake.

Pendekezo la pili nikuwa mamlaka ya rais ya punguzwe. Napendekeza kuwa mamlaka aliopewa Rais ya kuchagua mawaziri, makatibu wa wizara, na wakuu wote, yawe chini ya idhini ya Bunge. Inamainisha kuwa, Rais anapo pewa mamlaka kama ya kuchagua kama mawaziri, uteuzi wake uidhinishwe na Bunge, kwanza apewe approval ya Bunge ndiyo huyo aliochaguliwa apate kwanza kazi.
Pia napendekeza kuwa mamlaki ya Rais yakuvunja Bunge yaondolewe, kwa sababu hii inafanya wabunge kufanya kazi kwa uoga. Wanaogopa kuwa wakiende kinyume ya matakwa ya Rais, Rais anaweza kuvunja Bunge.

Pia napendekeza kuwa mamlaka ya Rais ya kutangaza vita yaondolewe na yawekwe katika chini ya idhini ya Bunge.

Pia napendekeza kuwa, msamaha unapendekezwa kuwa Rais akistafu hata kama amefanya vitendo vya uhalifu akiwa kwa

huduma, usikuwepo. Akifanya uhalifu aweze kuajibika kwa uhalifu anavyo fanya wakati yuko kwa huduma.

Pia napendekeza kuwa ile sheria inaomlazimu Rais kupata rasili mia ishirini na tano ya kura katika Mikowa mitano iondolewe. Napendekeza badala yake kuwa, kama Serikali ya majimbo itakubaliwa, Rais na mkuu ya majimbo, apate rasili mia hamsini na moja ya kura zote za urais na za ukuu wa jimbo zilizo pigwa, nakama kukosekana mtu aliepata rasili miya hamsini na moja ya kura zilizo pigwa, napendekeza kuwa kuwe uchaguzi wa pili, kati ya yule alieongoza kwa kura, na yule anayefuata nyuma yake.

Kuhusu Bunge, nina mapendekezo ya fuatayo. Napendekeza kuwa mamlaka ya Bunge ya kubadili sehemu yoyote ya Katiba kwa rasili mia ishirini na tano, yaondolewe kwani historia yetu inatuambiya kwa Bunge imeyatumia mamlaka haya vibaya.

Nasema hivi kwa sababu Bunge, limeundwa na Katiba. Bunge ni meundwana cha Katiba na haliwezi kuwa na mamlaka, itakua kimsingi makosa kwa Bunge kuwa na mamlaka ya kubadilisha Katiba, kwa hivyo kwa sababu ya historia yetu ya Bunge ya kutumia mamlaka hayo vibaya, na pia kwa sababu ya kuwa ni kinyume ya msingi wa Katiba kuwa juu ya Bunge napendekeza mamlaka haya yaondolewe kwa Bunge, na badala yake mamlaka yakubadilisha Katiba yapewe raia. Iwe ni kupitia kwa kura ya maoni.

Pia napendekesa kuwa Rais na mawaziri wasiwe wa Bunge, kwani kuwa kwao wa Bunge, kunaenda kinyume na msingi wa kugawanya mamlaka kati ya Serikali, Bunge na Mahakama.

Pia napendekeza kuwa katika sheria mpya ya Katiba tunawo pendekeza, kuwekwe sheria zinakazao ruhusu wangombeyaji huru wa viti vya udiwani, viti vya ubunge na viti vya urais.

Sheria inayo lazimu kila mgombeaji kudhaminiwa na chama iondolewe. Kwani kunabadhi yetu ambayo hatunge mkono, philosophia za vyama viloko mpaka sasa. Kwa hivyo Sheria hiyo inaenda kinyume na haki yetu ya kuchanganyikana.

Tena pendekezo ya kuwa Chama kitakacho unda Serikali kiwe kimepata asili miya hamsini na moja ya viti Bungeni. Asanteni.

**Com. Maranga –** Asante Bwana Jilo Martin. Asante. The next one is Muhamed Ali Bajila. Wapi Bwana Bajila? Muhamed? O.K. Dakika tano.

**Bwana Muhamed Ali Bajila –** Habari zenu wananchi? Na sina mengi manzake naona wengi washaongea na mengi washaongelewa lakini nitazungumuzia. Manzake naona pengine makarani wamechoka ndiyo wana harakisha wale wenye kuongea wapate kumaliza wale walio nayo ndani ya vichwa viao.

**Com. Maranga –** Sio hivyo kweli. Hatuja harakisha.

**Bw. Bajila –** Sio hivyo muwe uhuru mutuwache tuonge. Leo mumekuja na sisi pia tuna raha kumwona nyinyi mume tufikia mahali kama hapa, kwa hivyo tuko na mengi, hili mupate kuyajui yale ambayo yanatutatiza huku kwetu.

Na kama nitanzana kuyatoa jambo lakwanza ni lakwamba tutasungumuzia upande wa kilimo. Nafikiria wengi wameongea upande wa kilimo, na mimi nitazindi kuongezea. Kilimo ndiyo muongozo wa maisha ya jamii. Na kama ndiyo muongozo wa maisha wa jamii, tunaomba Serikali ichukulie muhimu sana kwa mukulima ili tuwe na hatua ya mbele. Kwa mategemeo ya kila mtu. Kwa hivyo tunaomba Serikali wapeyane mikopo katika jamii ili iwasaidie kuinuwa uchumi wa Kenya hii.

Na pili, ninaenda upande wa Elimu. Elimu, Tana River tunaonekana tuko nyuma sana, na kwa ajili ya hali ya kimaisha. Watu wa Tana River, wanajaribu kulima lakini mazawo yawo pia haya wasaidi, na kilimo ambacho kinatarajiwa sana ni maembe. Hiyo maembe piya unakuta hayana bei, Pamba pia halina bei. Hatujui watu wa Tana River nikitu gani kinge tusaidia ili tupate kuwafundisha vijana wetu. Kwa hivo, tunaomba kwa Serikali, vijana ambawo wameanzia darasa la kwanza mpaka la nane, Serikali watusaidie katika Kenya nzima iwe hawa vijana wanapewa elimu bure kama vile Mutukufu Rais ambavyo ameanzisha mwito huwo, Hayati Mzee Jomo Kenyatta.

Na tatu, tunaenda upande wa hali wa afya. Tana River, watu wengi wanaugua na hakuna matibabu yoyote ambawo yanamusadia mwananchi, kwa ajili tukiangalia madawa, Tana River inapatikana bei ya juu, na ukiangalia watu ambawo wanapatikana sehemu hio, hawana uwezo wa kununua madawa. Kwa hivo tunaomba Serikali pia vile vile, warudishe mvumo ule ule wa Hayati, alioanzisha wananchi kupewa dawa bure.

Tunaomba pia vile vile, ni ya nne hiyo, hali ya uchumi ume zorota, kwa hivo, tunaomba wananchi wasaidiwe na mikopo ili kuifadhi ardhi yawo kimazingira ili watajaribu kuwaleta wageni kutembelea sehemu zao ili wapate kujikuza. Nafikiria sina mengi ya zaidi, wako wengine pia watajazia pale nimeachia. Asante.

**Com. Maranga –** Asante Bw. Muhamed Ali. Asante kwa maoni yako na tumekupa muda kabisa umetoa maoni. Asante. Mwingine ambawo namwita ni Veronica Kwamboka. Wapi yeye. Veronica? Wapi Kwamboka huyo? Hayuko. Haya kuja utoe maoni.

**Omar Abdalla Dhadho** - Ningependa sasa kuchuwa nafasi hii kuwashukuru ma Commissioner wa Tume ya mageuzi ya Katiba kujitahidi kufika sehemu hii ya mwisho ambayo maranyingi inasahauliwa. Lakini wawo wamejitaidi wamefika mpaka kwenu, na wapokea maoni yenu. Nawashukuru sana. Ningependa pia kuwashukuru wananchi.

Meeting ended at 5.15 p.m.

&&&&&&&&&&&&&&&&&